TOFAUTI ZA UMENKE KATIKA MAZUNGUMZO YA DARASANI: UTAFITI KATIKA SHULE MBILI ZA UPILI, ZA MSETO WILAYA YA KILIFI – KENYA

NA:

NOAH, WAFULA CHRISTOPHER

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamili, (**M.A**), Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Egerton

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

Jan 2002

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu chochote kile.

Noah, Wafula Christopher — Tarehe 20/05/2002

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii walioteuliwa na Chuo Kikuu.

Dkt. Catherine Kitetu,
Idara ya Lugha na Isimu,
Chuo Kikuu cha Egerton. — Tarehe 20.05.02

Dkt. Beja S.K.
Idara ya Lugha na Isimu,
Chuo Kikuu cha Egerton. — Tarehe 21/5/2002

© HAKI ZA KUHIFADHI UCHAPISHAJI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kamwe kuiga tasnifu hii kwa mfumo wowote ule bila ya idhini ya mwandishi au/na Chuo Kikuu cha Egerton.

IKISIRI

Utafiti huu, umeshughulikia mazungumzo ya darasani kati ya mwalimu na wanafunzi ili kudhihirisha iwapo kuna usawa wa umenke kati ya wavulana na wasichana wanaoshiriki. Ingawa wanafunzi darasani huwa sawa, wanaisimu waliochunguza umenke darasani wanasema kuwa wasichana na wavulana wamekuwa wakihudumiwa tofauti katika mazungumzo ya darasani. Jambo hili, kulingana na utafiti katika nchi za ulaya, limechangia kutokuwepo kwa usawa, na mara nyingi wasichana huhasirika kwa kutopata nafasi ya kushiriki kikamilifu katika mazungumzo. Wasomi wanakubaliana kuwa mazungumzo ni kifaa muhimu sana katika upataji elimu. Kupitia mazungumzo, tunapitisha mawazo yetu kwa wengine, tunatalii mawazo mbalimbali, tunayathibitisha, na kuyafanya kuwa yetu. Utafiti huu ulichunguza na kubainisha ni nani wanaotawala mazungumzo ya darasani, na majukumu ya wahusika mbalimbali katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo hayo. Pia, utafiti huu, ulichunguza utaratibu wa kutoa nafasi za kuzungumza kwa wanafunzi na jinsi unavyoendeleza utawalaji wa mazungumzo. Utafiti huu ulijibana katika muktadha wa shule mbili za upili za mseto ambapo masomo ya Kiswahili na Kiingereza yalichunguzwa. Mtafiti alitumia misingi ya nadharia za Kiisimu za Uelemea Kike katika mtazamo wa Mwelekeo Lemevu. Matokeo ya utafiti huu yametuwezesha kufahamu vyema wanaotawala mazungumzo ya darasani, na sababu za hali hiyo. Ni matumaini yetu kuwa, utafiti huu utawafaidi walimu, mashirika mbalimbali yanayopigania usawa wa wanawake na wanaume, pamwe na wapangaji sera za elimu, hasa katika mijadala inayohusu ubora wa shule za mseto na zile zisizo za mseto.

SHUKRANI

Ama kwa kweli, kazi hii isingalifika kikomo chake kama si kwa juhudi na jitihada za watu mbali mbali ambao walinisaidia katika kuifanikisha. Kwanza kabisa, natoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi na walimu wangu Dkt. Catherine Kitetu na Dkt. Beja S.K. Hawa, licha ya kazi zao nyingi, waliisoma kazi yangu mara kwa mara, na hawakukawia kunipa mapendekezo ambayo yalinisaidia sana.

Shukrani zangu pia ziwafikie wahadhiri wangu; Bw. Furaha Chai, Bi. H. Mugambi, na Dkt. J. Kimemia. Hawa wote nawashukuru kwa msaada wao. Kamwe sitawasahau Dkt. A. G. Mwaro, na Mwalimu Onyango Ogolla kwa msaada wao ambao uliniwezesha kupata mada yangu ya utafiti.

Nawatolea pongezi waimbaji wa kanisa la Mtakatifu Thomaso - Kilifi kwa msaada wao walionipa. Mbali na kunifanyia mchango ambao uliniwezesha kupata hela za kujisajilisha katika Chuo Kikuu cha Egerton, hawakuchoka kunisaidia kila nilipokuwa na uhitaji. Vile vile, siwezi kuwasahau masahibu Paul, Amin, na Bw. Fondo ambao walijitolea kunisaidia kwa hali na mali. Mchango wao kwa kweli haukadiriki.

Mwalimu mkuu, Bi. Christine Kahindi, walimu; Bi Were, mabwana Mwangome, Nzai, Kombo, Kombe na Katana, sina budi pia kuwapa shukrani kwa ushirikiano wao nilipokuwa nyanjani. Kutokana na ushirikiano wao niliweza kukusanya data niliyohitaji kwa minajili ya tasnifu hii bila matatizo mengi.

Aidha namshukuru pia dada yangu Rose ambaye niliishi kwake kwa muda wote niliokuwa chuoni. Mungu ambariki. Msaada wa Stella, Salome, Grace, Jane na Jackline ulikuwa wa manufaa sana katika kufanikisha kazi hii. Ahsanteni nyote, Maulana awajazie thawabu

Mwisho, napenda kumshukuru Dorah Mitingi kwa kunipa moyo na kunichochea kila nilipoonekana kukata tamaa. Huyu sitamsahau kwa ushauri wake. Kuna watu mbali mbali ambao kwa njia moja au nyingine walinisaidia katika kufanikisha kazi hii. Iwapo baadhi yao sikuwataja hapa, nawaomba radhi. Ningependa wafahamu kuwa nawashukuru wote, tena kwa dhati popote walipo.

TABARUKU

Kwa wazazi wangu,

Noah Malala

Na

Emely Nyongesa.

Shukrani kwa kunilea na kunisomesha.

YALIYOMO

Ukurasa

UNGAMO ii

IKISIRI iv

SHUKRANI v

TABARUKU vii

DIBAJI YA MAJEDWALI x

SURA YA KWANZA 1

UJENZI WA UTAFITI 1

1.0 Utangulizi 1

1.1 Usuli wa mada 1

1.2 Somo la utafiti 4

1.3 Madhumuni ya utafiti 4

1.4 Maswali ya utafiti 5

1.5 Sababu na umuhimu wa utafiti 5

1.6 Upeo na mipaka ya utafiti 6

1.7 Maelezo ya Istilahi Adimu 7

1.8 Mbinu za utafiti 8

1.8.1 Uteuzi wa eneo la utafiti 8

1.8.2 Mbinu za ukusanyaji data 9

1.8.2.0 Utafiti awali 9

1.8.2.1 Utafiti kamili 10

1.8.3 Uchanganuzi wa data 12

1.9 Muhtasari 13

SURA YA PILI 14

YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA 14

2.0 Utangulizi 14

2.1 Utafiti katika mazungumzo na umenke 15

2.2 Utafiti kuhusu mazungumgo na umenke darasani. 17

2.2.1 Majukumu ya wahusika katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo. 18

2.3 Misingi ya nadharia 21

2.5 Muhtasari 23

SURA YA TATU 24

MATOKEO YA UTAFITI 24

3.0 Utangulizi 24

3.1 Utawalaji wa mazungumzo ya darasani 25

3.1.1 Idadi ya nafasi za kuzungumza, (Shule "A") 25

3.1.2 Idadi ya maneno yaliyochangiwa (shule "A") 26

3.1.3 Wastani wa maneno kwa kila nafasi (Shule "A") 27

3.1.4 Idadi ya nafasi walizopata Shule "B" 29

3.1.5 Idadi ya maneno yaliyochangiwa shule "B" 30

3.1.6 Wastani wa maneno kwa kila nafasi shule "B" 31

3.1.7 Shule "A" na Shule "B" 33

3.2 Majukumu ya wahusika katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo. 39

3.2.1 Majukumu ya wasichana na wavulana katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani. 40

3.2.2 Jukumu la mwalimu katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo. 43

3.3 Utaratibu wa kuteua wanafunzi katika mazunguzo ya darasani. 48

3.4 Muhtasari 49

SURA YA NNE 50

HITIMISHO 50

4.0 Utangulizi 50

4.1 Matokeo ya utafiti 50

4.2 Hitimisho ya utafiti 51

4.3 Matatizo yaliyokumba utafiti 52

4.4 Mapendekezo 53

VIAMBATISHO 54

MAREJELEO 96

DIBAJI YA MAJEDWALI

Jedwali 1 - Wanafunzi wanavyochangia shule "A".....25

Jedwali 2 – Wastani wa maneno kwa kila nafasi shule "A"..... 27

Jedwali 3 – Wanafunzi wanavyochangia shule "B" 29

Jedwali 4 – Wastani wa maneno kwa kila nafasi shule "B".....31

Jedwali 5 - Wanafunzi wanavyochangia shule "A" na "B".....33

Jedwali 6 - Wastani wa maneno kwa kila nafasi shule "A" na "B".....34

Jedwali 7 – Wanavyoinua mikono na kutumia nafasi zao 40

Jedwali 8 – Mwalimu alivyoteua wanafunzi 43

SURA YA KWANZA

UJENZI WA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Kazi hii imegawanywa katika sura nne. Sura ya kwanza imeshughulikia ujenzi wa somo la utafiti. Mbali na hayo, tumetaja pia madhumuni ya utafiti, sababu za kuchagua mada hii, na nadharia iliyotumika katika utafiti huu. Katika sura ya pili tumehakiki kazi mbali mbali zilizo na ukuruba au mwelekeo na utafiti wetu. Matokeo yamewasilishwa na kuchanganuliwa katika sura ya tatu. Mwisho tumetamatisha na kutoa mapendekezo yetu katika sura ya nne.

1.1 Usuli wa mada

Utafiti huu umeshughulikia swala la mazungumzo ya darasani. Katika mazungumzo hayo, utafiti huu umechunguza tofauti za umenke zinazodhihirika katika muktadha wa darasani. Kwa mujibu wa Swann (1992), tafiti nyingi zinazohusu hali ilivyo darasani zimedhihirisha hali mbalimbali za kiisimu na zisizo za kiisimu ambazo kwazo wasichana na wavulana huhudumiwa kitofauti. Lugha ni njia mojawapo ambayo hutumiwa kuendeleza tofauti hizi. Jambo hili husababisha kutokuwepo kwa usawa katika mazungumzo na hivyo hufanya kikundi kimoja kutawala na kufaidi mazungumzo ya darasani zaidi ya kingine. Hali hii huathiri kikundi kisichopata nafasi ya kuzungumza na mara nyingi, matokeo yakawa ni wavulana ndio wanaofaidika ilhali wasichana huhasirika.

Swala la usawa wa umenke ni swala ambalo limezua mwamko mpya katika miaka ya hivi punde miongoni mwa wasomi mbalimbali. Si usawa tu katika hali za kisiasa au

kiuchumi, bali pia katika hali za kijamii. Ni kutokana na mwamko huu ambapo tunaona kuwa ni jambo la muhimu kuchunguza usawa wa umenke katika mazungumzo ya darasani.

Mazungumzo ya darasani, ni eneo muhimu sana la kutafitiwa. Ni maoni ya wasomi wengi kama vile, Allwright na Bailey (1991), Marlland (1977), Coates (1993) na wengineo, kwamba mazungumzo ni kifaa muhimu sana katika upataji wa elimu. Mercer (1997:2),

> Katika jamii nyingi ulimwenguni kote, watu fulani hasa wazazi na walimu wamepewa majukumu fulani katika kuwasaidia wengine katika kuendeleza ufahamu na uelewa wa mambo. Hutarajiwa kuwasaidia kizazi kipya katika kuelewa mawazo mapya na kuwahami na vifaa vya kuendeleza mawazo hayo... wao hutimiza jukumu hili kwa njia nyingi, lakini njia ya muhimu na ya wazi zaidi ni kupitia kwa mazungumzo. (Tafsiri yangu)

Mwanalugha huyu anaendelea kudai kuwa walimu huweza kuwafundisha wanafunzi kwa njia ya mazungumzo. Kwa mujibu wa msomi huyu, ni vigumu kwa walimu kuwaelimisha wanafunzi kwa njia nyingine yoyote ile bila kuzingatia njia ya mazungumzo. Mercer (ibid) anakubaliana na wasomi wenzake niliowataja hapo mbeleni, kuwa mazungumzo ni muhimu sana katika upataji wa elimu. Bila ya mazungumzo ni vigumu sana kuelewa, kufafanua, na hata kuendeleza mawazo mbalimbali.

Kwa miaka zaidi ya ishirini na tano sasa, hali ilivyo darasani imebadilika na mazungumzo yamepewa umuhimu mkubwa katika upataji wa elimu. Hii ndiyo sababu huko Uingereza, kwa mfano, jambo hili limepewa uzito kupitia kwa sera na mifumo ya utaratibu wa kufundishia, ambapo inasisitizwa kuwa wanafunzi wapewe muda mrefu zaidi wa kuzungumza kuliko kuandika na kusoma. (Allwright na Bailey 1991).

Sera ya elimu huko Uingereza inasisitiza kuwa wanafunzi wapewe nafasi zaidi za kuuliza na kujibu maswali. Jambo hili linawezekana tu kupitia mazungumzo.

Hatuzungumzi kwa minajili tu ya kupitisha mawazo yetu kwa wengine, bali mazungumzo, vile vile, hutuwezesha kutalii mawazo mbalimbali, kuyathibitisha na kuyafanya yawe yetu (Marlland, 1977). Hata hivyo, Coates (ibid), anasema kwamba katika jamii hakuna usawa wa uzungumzi kati ya wanawake na wanaume. Yeye anadai kuwa wanawake huwa na nafasi chache katika mazungumzo. Marlland (ibid) anasema kwamba watoto, kwa kiasi fulani, hujifunza tabia za kimawasiliano kupitia mazungumzo ya darasani. Tunahofu kwamba, kuna uwezekano watoto huleta darasani, tabia wanazojifunza nyumbani hali ambayo pengine husababisha kundi moja kutoshiriki kikamilifu katika mazungumzo.

Utafiti huu umejikita katika muktadha wa shule za upili za mseto ambapo mazungumzo kati ya walimu na wanafunzi yalichunguzwa. Azma ya utafiti huu ilikiwa ni kudhihirisha ni nani, kati ya wasichana na wavulana, hutawala katika mazungumzo hayo. Pili, kuonyesha majukumu ya wahusika (wasichana, wavulana na walimu) katika kuendeleza hali hizi za umenke. Mwisho kuchunguza utaratibu unaoibuka wa kutoa nafasi za kuzungumza kwa wanafunzi na jinsi unavyoathiri utawalaji wa mazungumzo.

Kutokana na hali kwamba tafiti nyingi zinazohusu mazungumzo ya darasani zimefanyiwa ulaya, utafiti huu umelenga kutazama upya swala hili, katika mazingira ya nchi za Kiafrika na hususan, Kenya na kuona iwapo pataibuka matokeo sawa na hayo ya awali au la. Utafiti huu unatupa msingi mzuri wa kuelewa maswala haya nchini Kenya.

1.2 Somo la utafiti

Hali ilivyo ni kwamba katika jamii, hakuna usawa wa umenke na huenda ikawa hali hii pia inadhihirika darasani hivyo kuathiri wanafunzi katika upataji wa elimu. Kwa sababu hakuna utafiti wa kina uliofanywa kuhusu swala la mazungumzo ya darasani na umenke katika Kenya na Afrika kwa jumla, tulioweza kupata, utafiti huu ulikuwa na azma ya kujaza mwanya huu kwa kuchunguza ni nani miongoni mwa wasichana na wavulana hutawala mazungumzo ya darasani. Utafiti huu pia umechunguza hali zinazosababisha utawalaji wa mazungumzo hayo kwa kuonyesha majukumu ya wahusika (wasichana, wavulana na walimu) katika kuendeleza hali hii. Aidha tumechunguza utaratibu unaoibuka wa kutoa nafasi za kuzungumza na jinsi unavyoathiri utawalaji wa mazungumzo ya darasani, kwani maswala haya hayakujulikana hapo awali.

1.3 Madhumuni ya utafiti

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni:

1. Kuonyesha ni nani, kati ya wavulana na wasichana, wanatawala mazungumzo ya darasani
2. Kudhihirisha majukumu ya wahusika (wasichana, wavulana, na walimu) katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani.
3. Kubainisha iwapo utaratibu unaotumika wa kutoa nafasi za kuzungumza huendeleza na kuathiri utawalaji katika mazungumzo ya darasani.

1.4 Maswali ya utafiti

Utafiti huu umejibu maswali matatu makuu. Maswali haya ni:

1. Kati ya wasichana na wavulana darasani, nani wanatawala mazungumzo?
2. Ikiwa kuna hali ya utawalaji katika mazungumzo ya darasani, je, wahusika (wasichana, wavulana na walimu) wana majukumu gani katika kuendeleza hali hii?
3. Je, utaratibu unaoibuka, wa kupeana nafasi za kuzungumza, huendeleza na huathiri vipi hali ya utawalaji wa mazungumzo ya darasani?

Uteuzi wa maswali haya umetuelekeza na kutusaidia katika kupangilia kazi yetu ili kutimiza malengo ya utafiti.

1.5 Sababu na umuhimu wa utafiti

Utafiti huu umechochewa na umuhimu wake. Uchunguzi na utafiti juu ya maswala ya umenke ni jambo ambalo limetiliwa mkazo katika miaka ya hivi punde, hususan, katika nchi za Kimagharibi. Nyingi ya tafiti hizi zimebainisha kwamba wanawake wana nafasi chache za kujieleza wanapokuwa katika mazungumzo na wanaume. Jambo hili huathiri uelewa na uthibitishaji wa mawazo.

Katika mipango ya maendeleo mwaka wa 1996, serikali ya Kenya ilisisitiza kwamba elimu ndicho chombo cha pekee ambacho kingeweza kupunguza hali ya kutokuwepo kwa usawa wa umenke katika maeneo mbalimbali ya kijamii. Serikali ilisisitiza kufutiliwa mbali kwa hali zinazodhihirisha ubaguzi wa umenke katika vitabu vya elimu na kusisitiza elimu bora kwa msichana, kwa kumweka katika mazingira bora ya kielimu. Ingawa serikali haikutaja swala la mazungumzo ya darasani kinagaubaga, tafiti nyingi za kiisimu zimedhihirisha kuwa mazungumzo ni muhimu katika kujiendeleza

kielimu, kitabia na hata kifikra (Marlland, ibid). Ndiposa ikawa ni muhimu kutafiti swala la tofauti za umenke katika mazungumzo ya darasani ili kubainisha iwapo usawa wa umenke upo.

Kwa mujibu wa Delamont (1980), tofauti za umenke au kutokuwepo kwa usawa wa umenke, kunaweza kuwa na athari mbaya kwa wasichana na hata wavulana katika maendeleo yao ya kielimu. Hali hii inaweza kuwaathiri wanafunzi, katika masomo yao na jinsi watakavyohusiana na wanajamii kwa jumla. Delamont anaendelea kusema kuwa shule kwa kiasi fulani zinachangia hali hii ya kuendeleza tofauti za umenke. Hivyo ilikuwa ni muhimu kutafiti swala hili.

Nchini Kenya, ni watafiti wachache tu ambao wameshughulikia swala hili la mazungumzo na umenke. Isitoshe, hata hao wachache, wengine wao si wanaisimu, hawalishughulikii swala hili kupitia mtazamo wa kiisimu na misingi ya umenke.

Utafiti huu, ni matumaini yetu kuwa utawafaidi wapangaji wa sera za elimu hasa kuhusu uwepo wa shule za mseto, pia utawafaidi walimu (hasa katika kuelewa umuhimu wa kuwahusisha wanafunzi wote katika mazungumzo). Utafiti huu pia umetoa mapendekezo kuhusu sera na mipango ya elimu. Zaidi ya hayo, utafiti huu umetoa mchango kwa wasomi katika nyanja ya lugha na umenke, na hususan, katika eneo la mazungumzo ya darasani Kenya.

1.6 Upeo na mipaka ya utafiti

Utafiti huu umejikita katika muktadha wa mazungumzo ya darasani kati ya mwalimu na wanafunzi, katika shule za upili za mseto wilayani Kilifi. Imelazimu utafiti kufanyiwa katika shule za mseto kwa sababu unahusisha wasichana na wavulana.

Vipindi vinane katika masomo ya Kiingereza na Kiswahili hasa katika vipengele vya sarufi, ufahamu na fasihi vilichunguzwa. Vipengele hivi vilichaguliwa kwa sababu vinahusisha mazungumzo miongoni mwa washiriki (walimu na wanafunzi). Masomo ya Kiswahili na Kiingereza yalichaguliwa kwa sababu ni masomo ya lazima kwa kila mwanafunzi, na hivyo, kila mwanafunzi darasani anashiriki. Pili, kwa sababu utafiti huu unahusu maswala ya lugha, ilikuwa ni muafaka kuchunguza masomo ya lugha.

Mtafiti alijibana katika muktadha wa darasani wakati mwalimu alipokuwa akifundisha. Hivyo, mazungumzo yaliyochunguzwa ni yale yaliyotokana na muktadha huu.

1.7 Maelezo ya Istilahi Adimu

Istilahi zifuatazo zimefafanuliwa kwa maana na jinsi zilivyotumika katika utafiti huu.

i. **Umenke:**

Istilahi hii imetumika kutofautisha mwanamume na mwanamke kutokana na misingi ya kijamii ambapo wanaodhihirisha hali za kiume huitwa wanaume ilhali wanaodhihirisha hali za kike huitwa wanawake.

ii. **Mtazamo Mwelekeo Lemevu:**

Mtazamo wa kinadharia unaosisitiza kuwa tofauti za kisutua miongoni mwa watu, ndicho chanzo cha tofauti za umenke katika matumizi ya lugha ambapo wanaume hutawala.

iii. **Tofauti za umenke**:-

Hali zinazodhihirika au kujengeka katika hali mbalimbali, mazungumzo yakiwemo. Hali hizi zinatokana au husababishwa na tofauti ilioko kati ya wanawake na wanaume.

iv. **Kutawala mazungumzo**

Istilahi imetumika kumaanisha ile hali ya kuchangia zaidi au kuchukua nafasi nyingi zaidi ya wengine katika mazungumzo yanayohusisha zaidi ya mtu mmoja.

v. **Mazungumzo ya darasani**

Haya ni yale mazungumzo kati ya mwalimu na wanafunzi yanayojiri katika muktadha wa darasani wakati mwalimu anapofundisha.

1.8 Mbinu za utafiti

1.8.1 Uteuzi wa eneo la utafiti

Kwa kutumia uteuzi nasibu, shule nane (8) za upili za mseto ziliteuliwa. Baada ya kuwaandikia barua walimu wakuu wa shule hizi, ni walimu watano pekee waliojibu. Kati ya shule tano (5) ambazo zilijibu kupitia kwa walimu wakuu wa shule hizo, ni shule mbili (2) tu zilizokuwa na idadi iliyokaribiana ya wasichana na wavulana katika madarasa ambayo mtafiti alinuia kufanya utafiti. Katika utafiti huu, ilikuwa ni muhimu kuwepo kwa idadi sawa au iliyokaribiana ya wasichana na wavulana. Iwapo kikundi kimoja (aidha wsichana au wavulana) kingekuwa na wahusika wachache basi ingekuwa dhahiri kuwa pengine kikundi hicho kwa vyovyote vile kingetwaliwa.

Shule zilizoteuliwa ziko katika wilaya ya Kilifi. Shule moja (shule "A") iko kijijini hali shule ya pili (shule "B") ni ya mjini. Wilaya hii imechaguliwa kwa sababu iko katika mkoa wa Pwani ambako kwa miaka mingi, shule zimekuwa hazifanyi vyema katika mitihani ya kitaifa zikilinganishwa na mikoa mingine,, kama vile, mkoa wa Kati. Tatizo la umenke ni mojawapo ya matatizo mengi yanayokumba mkoa huu na huchangia kutofanya vyeme kwa wanafunzi katika mitihani ya kitaifa. Hivyo, ni muhimu utafiti unaohusu maswala ya kielimu kufanywa katika mkoa huu. Aidha, kwa sababu mtafiti anaishi katika sehemu hiyo, ilikuwa nafuu kwake hasa katika hali za usafiri.

Kwa kutumia uchunguzi, jumla ya vipindi vinane vya masomo ya Kiingereza na Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa kidato cha tatu na cha nne vilichunguzwa. Vidato hivi viliteuliwa kwa sababu wanafunzi katika vidato hivi huwa wamekaa shuleni muda mrefu zaidi ya wengine, wamezoena, na hivyo basi hakuna sababu ya kusema kwamba wao hawachangii katika mazungumzo kwa sababu hawajazoeana. Pia tulichagua vidato vya tatu na nne ili tuweze kupata data ya kutosha.

1.8.2 Mbinu za ukusanyaji data

1.8.2.0 Utafiti awali

Utafiti huu ulifanywa nyanjani na maktabani. Kabla ya kuanza utafiti kamili, mtafiti alifanya utafiti awali katika eneo la utafiti ambapo aliweza kubainisha idadi ya wasichana na wavulana katika kila darasa alilonuia kuingia na pia kujaribu mbinu na vifaa vya ukusanyaji data. (Angalia kiambatisho x uk. 65, ili kujua idadi ya wasichana na wavulana katika kila darasa).

Utafiti awali ulisaidia sana hasa katika kuteua shule ambazo zilifanyiwa utafiti. Mwanzoni shule tano (5) zilikuwa zimeorodheshwa lakini baada ya kutembelea shule hizi, ilibainika kwamba shule nyingine zilikuwa na idadi ndogo sana ya wasichana. Pia ilibainika kwamba vipindi ishirini na nne (24) ambavyo ilikuwa imepangwa vichunguzwe vilikuwa vingi mno, kwa hivyo, vipindi vinane (8) pekee vilichunguzwa.

1.8.2.1 Utafiti kamili

Utafiti huu, kama nilivyosema hapo awali, ulihusisha shule mbili za mseto. Shule "A" ni ya kijijini ilhali shule "B" ni ya mjini. Jumla ya wanafunzi mia moja thelathini na mbili (132) walishiriki. Kati ya hawa, wanafunzi sitini na saba (67) walikuwa wasichana, ilhali sitini na tano (65) walikuwa wavulana. Mbali na hao walimu wanane pia walishirikishwa katika utafiti huu. Walimu saba (7) walikuwa wanaume ilhali mwalimu mmoja alikuwa wa kike. Walimu hawa walifahamishwa kwamba lego la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza jinsi hali inavyoendelea darasani na jinsi mwalimu anavyohusisha wanafuzi wakati anapofundisha.

Jambo hili la kuwajulisha walimu lengo la utafiti kwa kiasi kikubwa lilisaidia sana hasa katika kupata data ya kutosha kwani walimu waliwahusisha wanafunzi katika masomo walipokuwa wakifundisha. Hata hivyo kwa kiasi kidogo, jambo hili pia lilikuwa na matatizo, kwani kuna walimu wengine ambao walidhani walikuwa wakichunguzwa na hivyo basi mwazoni mwa utafiti hawakuwa na ushirikiano mzuri na mtafiti.

Katika kufanikisha utafiti huu, mbinu kadha wa kadha zilitumiwa katika ukusanyaji wa data. Kwanza, imetumika mbinu ya uchunguzi. Katika kufanikisha matumizi ya mbinu hii ya uchunguzi, mtafiti alikaa pembeni, mbele ya darasa. Akiwa mbele, mtafiti aliweza kuona wanafunzi wote katika darasa, na hivyo basi ilikuwa rahisi kwake kuchunguza maswala kadha wa kadha aliyokuwa ameyaorodhesha. Haya ni kama kama

vile; ni kina nani wananyosha mikono, kina nani wanateuliwa kuzungumza, nani wasionyosha mikono na kadhalika.

Mtafiti, alichunguza na kuhesabu idadi ya wasichana na wavulana walioinua mikono na wale ambao hawakuinua mikono wakati mwalimu alipouliza swali. Jambo hili lilikuwa muhimu, kwani lilituwezesha kujua wale waliokuwa na hamu ya kuzungumza hivyo basi kutusaidia katika kujua majukumu ya wavulana na wasichana katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo. Pia, katika hali hiyo ya kujua majukumu, mtafiti alichunguza na kuhesabu idadi ya wasichana na wavulana wasiojibu maswali hata baada ya kuteuliwa na mwalimu.

Vile vile, mtafiti alichunguza na kuhesabu idadi ya nafasi za kuzungumza walizopata wasichana na wavulana. Jambo hili liliwezekana kwa matumizi ya shajara za nyanjani. Kila wakati mwalimu alipouliza swali, mtafiti alikuwa makini kujua nafasi ya kuzungumza ilipewa mvulana au msichana. Mwisho mtafiti alijumlisha nafasi zote walizopata wasichana na zile walizopata wavulana. Jambo hili, lilisaidia katika kubainisha nani wanaotawala mazungumzo ya darasani. Viambatisho ii – viii (ukurasa wa 55 - 63) vinaonyesha data ya aina hii. Hii ikiwa ni data iliyotokana na uchunguzi wakati mwalimu yuko darasani akifundisha.

Kinasa sauti kilitumika katika kunasa mazungumzo yaliyojiri. Kinasa sauti hiki kilisimamishwa pembeni mbele ya darasa. Baadaye tulinakili mazungumzo hayo kutoka katika kanda za sauti (viambatisho xi – xviii 66 – 93) vinadhihirisha data iliyotokana na kanda za sauti). Jambo hili lilituwezesha kuhesabu idadi ya maneno yote yaliyochangiwa na wavulana na idadi ya maneno yaliyochangiwa na wasichana. Kutokana na hayo, tuliweza kupata wastani wa maneno kwa kila nafasi kwa wasichana na wavulana. Jambo hili lilituwezesha kujua iwapo wasichana na wavulana walitumia nafasi walizopata kwa

mapana wala si kujibu kwa neno moja moja tu. Kutokana na mbinu hizi, data tuliyopata ilikuwa ni shajara za nyanjani na kanda za sauti

Mbali na hayo, mtafiti pia alihesabu idadi ya wavulana na wasichana walioteuliwa kuzungumza wakati kulipokuwa na idadi sawa ya wavulana na wasichana waliokuwa wameinua mikono. Jambo hili lilisaidia katika kujua jukumu la mwalimu katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo.

Kwa mukhtasari, kulikuwa na data ya aina mbili. Kwanza, data iliyopatikana kutokana na uchunguzi, ambapo vipengee kadha wa kadha nilivyovitaja hapo juu vilichunguzwa. Mfano wa data hii ni kama inavyodhihirika katika viambatisho ii - viii ukurasa wa 55 – 63. Pili, kulikuwepo na data iliyopatikana kutokana na kanda za sauti. Mtafiti kwa kutumia kinasa sauiti, alinasa mazungumzo yote yaliyojiri darasani wakati mwalimu alipokuwa akifundisha. Ni kutokana na data hii ambapo mtafiti aliweza kuhesabu idadi ya maneno iliyochangiwa na kila kikundi (wavulana na wasichan). Mfano wa data hii ni kama inavyodhihirika katika viambatisho xi – xviii ukurasa wa 66 – 93.

1.8.3 Uchanganuzi wa data

Mtafiti alichanganua data iliyopatikana, kwanza, kwa kuhesabu idadi ya nafasi walizopewa wasichana na wavulana katika kujibu maswali ya mwalimu. Pili, jinsi wasichana na wavulana walivyoshiriki katika mazungumzo kwa kuinua au kutoinua mikono. Tatu, jinsi mwalimu alivyotoa nafasi za kuzungumza kwa wanafunzi aidha kwa kuteua walioinua mikono au hata wale wasioinua mikono. Kama nilivyosema hapo mbeleni, mtafiti alizitafsiri kanda za sauti na kuziweka katika hali ya maandishi. Jambo hili lilimuwezesha mtafiti kuhesabu idadi ya maneno yaliyochangiwa na wavulana na idadi ya maneno yaliyochangiwa na wasichana.

Mwisho mtafiti alifanya hesabu na kupata, kwa misingi ya mbinu ya msambao mara-tokezi, wastani wa maneno kwa kila nafasi kwa wasichana na wavulana. Kigezo hiki hasa ndicho kilichotumika katika kujua ni nani wanatawala mazungumzo ya darasani, hili likiwa swali kuu la utafiti huu. Vigezo vingine kama vile, nani waliokuwa wakiinua au kutoinua mikono, nani walipata nafasi lakini hawakuzitumia, mwalimu aliteua kina nani zaidi n.k, vimetumika kwanza, katika kubainisha majukumu ya wanafunzi na mwalimu katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo. Pili, kujua utaratibu unaojitokeza wa kuteua wanafunzi katika mazungumzo na jinsi unavyoathiri utawalaji wa mazungumzo hayo.

1.9 Muhtasari

Katika sura hii, tumeweza kutoa mwanga kuhusiana na mada yetu ya utafiti ambayo ni: **Tofauti za umenke katika mazungumzo ya darasani: utafiti katika shule mbili za upili, za mseto wilaya ya Kilifi – Kenya.**

Mbali na kuangazia majukumu ya utafiti huu, pia tumeeleza sababu na umuhimu wa kuchagua mada hii. Sababu mojawapo ikiwa ni kwamba hakuna utafiti wa kina tulioweza kupata kuhusu swala la mazungumzo ya darasani na umenke, na kuwa umuhimu wa utafiti huu ni kwamba utawafaidi walimu, wapangaji sera za elimu na wasomi kwa jumla.

Vile vile, tumeelezea mbinu mbalimbali ambazo zilitumika katika kufanikisha utafiti huu. Katika sura inayofuata, tunachunguza kazi au tafiti za wasomi mbalimbali ambazo kwa njia moja au nyingine, zilisaidia sana katika kufanikisha utafiti huu. Sura hii, imejenga somo la utafiti na kuweka msingi wa kueleweka kwa sura zinazofuata, na utafiti wenyewe kwa jumla

SURA YA PILI

YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumehakiki kazi za awali za wasomi kadha wa kadha ambazo zina ukuruba na utafiti huu. Katika hali hii, tumechunguza kazi hizi kwa undani na kudhihirisha mapengo yanayojitokeza ambayo yamejazwa na utafiti huu. Katika miaka ya hivi punde, mada hii 'lugha na umenke' imeshughulikiwa na watafiti wengi ambao wamejaribu kuonyesha uhusiano uliopo kati ya njia za kutumia lugha, na majukumu ya kijamii ya wanawake na wanaume wanaotumia lugha hiyo. Kutokana na hayo, kumezuka maswali mengi ambayo yamezua mshawasha na mjadala katika nyanja hii ya lugha na umenke.

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza iwapo kuna usawa wa umenke katika matumizi ya lugha na katika mazungumzo ya darasani. Kwa mujibu wa Coates (1993), swala kwamba wanawake na wanaume hutofautiana katika tabia zao za kimawasiliano ni jambo ambalo sasa limekubalika kiisimu. Lililobaki ni kutafiti tofauti hizi katika miktadha mbalimbali na kuchunguza athari za tofauti hizi kwa wahusika katika mawasiliano.

Sura hii imegawanywa katika sehemu tatu kuu. Katika sehemu ya kwanza, kazi zinazohusu mazungumzo, na umenke kwa jumla, zimechunguzwa kwa kuzingatia mazungumzo baina ya wanawake na wanaume, katika miktadha tofauti. Sehemu ya pili ya sura hii, imetathmini tafiti zilizofanywa kuhusiana na mazungumzo na umenke katika muktadha wa darasani. Katika sehemu hii, tuliweza pia kuchunguza jinsi utawalaji wa

mazungumzo ulivyoendelezwa na jinsi wanafunzi walivyoteuliwa au kupewa nafasi za kuzungumza darasani. Mwisho, sehemu ya tatu ya sura hii imejadili nadharia iliyotumika katika kufanikisha utafiti huu.

2.1 Utafiti katika mazungumzo na umenke

Wasomi mbalimbali kutoka nje ya Afrika wamejaribu kufanya utafiti kuhusu swala hili la mazungumzo na umenke kwa kuchunguza mazungumzo kati ya wanaume na wanawake. Tumetumia tafiti hizi kama muelekeo au vidokezo katika utafiti huu, ili kuelewa ni kwa kivipi wanawake hunyimwa nafasi katika mazungumzo.

Wardhaugh (1986) anasema kuwa katika mazungumzo kati ya wanawake na wanaume, kunadhihirika uhusiano wa 'kawaida' wa kisutua unaoendelezwa katika jamii, ambapo wanaume huonekana kuwa wenye nguvu ilhali wanawake hawana nguvu. Anaendelea kuwa, hali hii huwa hivyo kwa sababu hivyo ndivyo walivyojamiishwa.

Utafiti huu wa sasa haukuchunguza ni vipi wanawake au wanaume huzungumza, au kutumia vigezo vya kiimbo, au vijiswali kama ilivyotumiwa na watafiti wa awali katika kudhihirisha utawalaji. Hata hivyo, utafiti huu ulitumia misingi iliyowekwa na watafiti hawa kwamba, kuna tofauti kati ya uneni wa wanawake na wanaume, katika kuchunguza jinsi tofauti hizi zinavyoendeleza utawalaji katika mazungumzo ya darasani.

Utafiti wetu, hivyo basi ulipiga hatua zaidi kwa kuchunguza ni kikundi gani hutawala mazungumzo ya darasani, na wahusika wana jukumu gani katika kuendeleza utawalaji huo. Hali hii iliwezekana kwa kuchunguza nafasi za kuzungumza za kila muhusika na idadi ya maneno inayochangiwa na kila muhusika.

Zimmerman na West (1975) walichunguza mazungumzo kati ya wanawake na wanaume. Hawa katika utafiti wao waligundua kwamba wanawake na wanaume

wanapokuwa katika mazungumzo, wanaume huonekana ndio wanaozungumza sana. Wanawake huonekana kuwa wapole na hutumia muda mwingi kusikiza wala si kuzungumza, wakilinganishwa na wanaume.

Wasomi hawa wanaendelea kusema kuwa wanaume huonekana kuwakata kauli wanawake mara kwa mara. Hali hii inaonyesha wazi kwamba wanaume ndio wanaotawala mazungumzo kati yao na wanawake. Utafiti wetu haukutumia kigezo cha ukataji kauli bali ulitumia vigezo kama vile idadi ya maneno inayochangiwa na kila mwanafunzi na idadi ya nafasi za kuzungumza za kila mwanafunzi, katika kudhihirisha nani anatawala mazungumzo ya darasani.

Kwa kiasi fulani, matokeo ya Zimmerman na West (ibid) kuwa wanawake hutumia muda wao mwingi kusikiliza, yaliweza kudhihirika katika utafii huu pia. Hivyo kusababisha wavulana kutawala mazungumzo ya darasani. Utafiti wetu haukukomea hapo bali, mbali na kushughulikia swala hili katika muktadha wa madarasa ya shule za upili, ulipiga hatua zaidi kwa kuangalia majukumu ya wahusika katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani.

Kramer (1979), alichunguza jinsi wanawake walivyowasilishwa katika vibonzo. Mtafiti huyu, alikusanya makala ya vibonzo vya gazeti la *'The New York'* lililochapishwa kati ya Februari 17 na Mei 12, 1973. Uchunguzi wake ulidhihirisha kwamba, mbali na kuwa wanaume na wanawake katika vibonzo hivi walizungumzia juu ya mada tofauti, wanaume walizungumza mara mbili zaidi ya wanawake. Hali hii inadhihirisha kwamba wanaume walitawala mazungumzo hayo.

Utafiti huu wa Kramer kama ulivyotajwa hapo mbeleni, uliweka msingi thabiti wa utafiti huu, msingi ambao tumeujenga kadri ya uwezo wetu, hasa katika kauli kuwa wanaume ndio wanaotawala mazungumzo. Kramer hakufanya uchunguzi wake katika

muktadha maalum kama vile darasani au sokoni. Mtafiti huyu vile vile, hakutumia hali halisi za kimaisha, bali alitumia tu vibonzo. Utafiti wetu ulipiga hatua zaidi kwa kuchunguza muktadha maalum wa shule na hususan katika darasa, hii ikiwa ni hali halisi ya kimaisha.

2.2 Utafiti kuhusu mazungumgo na umenke darasani.

Shule ni mahali ambapo kuna midahalo mingi na maingiliano kadha wa kadha ya kiisimu au kimazungumzo. Maingiliano haya mara kwa mara, hutumika katika kuendeleza maswala kadha wa kadha ya umenke.

Kutokana na hali ya kutokuwepo kwa picha kamili kuhusu swala la utawalaji wa mazungumzo kati ya wasichana na wavulana, ilikuwa ni muhimu kufanyia utafiti swala hili katika muktadha wa nchi za Kiafrika, na hasa Kenya ambapo ni utafiti mchache uliofanywa kuhusiana na jambo hili.

Katika utafiti wake, Beatie (1981) alichunguza mihadhara ya wanafunzi wa Chuo Kikuu. Yeye aligundua kwamba wanafunzi wa kike walishiriki kikamilifu katika mazungumzo na kuchangia sawa sawa na jinsi wanafunzi wa kiume walivyochangia. Hata hivyo, imedhihirika kuwa, matokeo haya yalitofautiana na yale ya watafiti wengine. Swann na Graddol (1988), wanasema kuwa ingawaje imekuwa ikiaminiwa kwamba wanawake ndio wanaozungumza sana, tafiti nyingi zimedhihirisha ni wanaume ndio wanaotawala mazungumzo.

2.2.1 Majukumu ya wahusika katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo.

Katika kuchunguza jinsi utawalaji unavyoendelezwa, Spender (1982) anasema kuwa iwapo wavulana wanatawala mazungumzo ya darasani, wanafanya hivyo kwa usaidizi wa mwalimu. Mwanaisimu huyu anaendelea kusema kuwa, walimu huwateua na kuwasikiliza zaidi wavulana na hivyo basi kuwatia moyo zaidi wa kuendelea kuzungumza. Kwa mujibu wa Spender, ni vigumu sana kwa mwalimu kuwapatia wasichana na wavulana nafasi sawa za kuzungumza. Kwa kiasi fulani, utafiti huu wetu umethibitisha kuwa inawezekana mwalimu kuwapatia wasichana na wavulana nafasi sawa za kuchangia katika mazungumzo ya darasani.

Katika mradi uliohusisha wasichana, katika Sayansi na Teknolojia huko Manchester, Whyte (1986), alichunguza madarasa ya sayansi, ambapo alijaribu kuwashawishi walimu kutumia muda wao darasani kwa kuwapatia wasichana na wavulana nafasi sawa za kuzungumza. Aligundua kwamba, kwa kushawishiwa, walimu waliweza kuwapatia wasichana na wavulana muda sawa katika mazungumzo ya darasani, na hivyo kuwashirikisha wote kikamilifu, katika maswala mbalimbali ya darasani. Hali hii ilisababisha wasichana na wavulana kuchangia sawa kwa sawa katika mazungumzo hayo.

Hata hivyo mwalimu mmoja alipohojiwa baadaye, alisema kwamba alijihisi kama ambaye alitumia asilimia tisini (90%) ya wakati wake kwa wasichana! Usemi huu kwa mujibu wa mwalimu huyu unadhihirisha kwamba, kuwapatia wasichana nafasi nyingi za kuzungumza darasani, halikuwa jambo la kawaida.

Utafiti wetu haukutumia mkondo huu wa ushawisihi, kwani, mbali na kutaka kujua ni nani wanatawala mazungumzo ya darasani, utafiti huu pia ulikuwa na lengo la

kubainisha jukumu la mwalimu katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani bila ya yeye kushawishiwa kuwapatia wanafunzi nafasi sawa.

Katika utafiti wao huko Uingereza, French na French (1984), walichunguza jinsi walimu na wanafunzi wa shule za msingi walivyojihusisha katika mazungumzo. Walitafiti njia walizotumia walimu katika kuwapatia wanafunzi nafasi za kuzungumza. Watafiti hawa waligundua kuwa, walimu waliwapendelea zaidi wanafunzi waliotoa majibu ambayo yalionekana kuwa ya kuvutia (na hivyo kuwapatia nafasi zaidi za kuzungumza). Kwa sababu wavulana ndio waliotoa majibu ya aina hiyo, walipata nafasi nyingi zaidi za kuzungumza na hivyo kutawala mazungumzo.

French na French (ibid) walitumia kikundi kidogo tu cha wanafunzi na hivyo basi matokeo haya hayawezi kuchukuliwa kama yanawakilisha hali ilivyo. Isitoshe, wao walisema tu kuwa walimu waliwapendelea wavulana lakini hawakuangalia au kuchunguza majukumu ya wanafunzi katika kuendeleza hali hii. Utafiti huu umetumia zaidi ya darasa moja katika shule mbili tofauti hivyo kujumuisha kundi kubwa la wanafunzi.

Swann na Graddol (1988), walichunguza jinsi wanafunzi walivyopata nafasi zao za kuzungumza. Hawa walitumia vikundi viwili vidogo vya wanafunzi wa shule ya msingi. Kikundi cha kwanza kilijumuisha wasichana watatu, wavulana watatu na mwalimu mmoja wa kike ilhali kikundi cha pili kilijumuisha wavulana wanne, wasichana wanne, na mwalimu mmoja wa kike. Wanafunzi wote walikuwa na umri wa kati ya miaka tisa (9) na miaka kumi na moja (11).

Watafiti hawa waligundua kwamba wavulana walichangia zaidi katika idadi ya maneno na hata idadi ya nafasi za kuzungumza. Jambo muhimu walilogundua ni kwamba tabia ya mwalimu ya kuwaangalia wavulana zaidi kila alipouliza swali iliwasaidia

wavulana kuchangia zaidi katika mazungumzo. Waligundua kuwa, wavulana waliweza kuinua mikono yao haraka zaidi kuliko wasichana hivyo basi kupata nafasi zaidi.

Utafiti huu wa Swann na Graddol ulitumia wanafunzi wachache, tena wa shule ya msingi. Utafiti wetu umepiga hatua zaidi na kuchunguza tabia za wanafunzi, kama vile, kutoinua au kuinua mikono, na kujibu au kutojibu maswali katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani. Isitoshe, utafiti wetu, tofauti na ule wa Swann na Graddol, umetumia idadi kubwa ya wanafunzi, tena wa shule za upili.

Utafati mwingine tulioweza kurejelea ni ule wa Sadker na Sadker (1985). Wasomi hawa, walitafiti mbinu za kufundisha zinazotumiwa na walimu. Katika utafiti wao wa zaidi ya madarasa mia moja, waligundua kwamba kwa kadiri, wavulana walizungumza mara tatu zaidi ya wasichana. Aghalabu wavulana ndio waliojibu maswali zaidi wakilinganishwa na wasichana, na mwisho, walimu walikubali zaidi majibu ya wavulana kuliko ya wasichana.

Watafiti hawa hawakuendelea mbele zaidi na kuchunguza majukumu ya wanafunzi na walimu katika kuendeleza hali hii ya kutokuwepo kwa usawa wa kimazungumzo. Aidha hawakushughulikia utaratibu uliotumika wa kuepeana nafasi za kuzungumza na jinsi ulivyoendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani. Utafiti huu uliweza kujaza pengo hili.

Nchini Kenya, ni watafiti wachache tu ambaowameshughulikia swala hili la mazungumzo ya darasani. Juma (1991), alichunguza muundo wa mdahalo wa darasani. Huyu, aligundua kuwa katika mdahalo wa darasani, jukumu la mwalimu lilikuwa ni kuanzisha mazungumzo na kuwafahamisha wanafunzi. Katika utafiti huu, ilijitokeza wazi wazi kuwa mwalimu ana jukumu kubwa sana katika mazungumzo ya darasani. Utafiti wa Juma haukujishughulisha na maswala ya umenke. Utafiti huu wa sasa utachunguza ni

kwa jinsi gani jukumu hili la mwalimu huchangia katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani.

Katika utafiti wake uliohusisha njia za mdahalo katika darasa la Sayansi, Muthwii (1988), alichunguza njia zilizotumika katika kuuliza maswali katika somo la Kemia. Kwa kuchunguza vipindi arubaini, mtafiti huyu aligundua kwamba, mwalimu kwa kiasi kikubwa ndiye aliyetawala mazungumzo ya darasani. Utafiti huu wa Mutwii haukujishughulisha na maswala ya umenke. Ingawaje katika utafiti wake ilibainika kuwa mwalimu ndiye aliyezungumza kwa kiasi kikubwa, mtafiti huyu hakuchunguza na kubaininsha ni nani kati ya wavulana na wasichana wanatawala mazungumzo ya darasani.

2.3 Misingi ya nadharia

Utafiti huu umeongozwa na misingi ya nadharia ya Kiisimu-Uelemea Kike, hasa katika Mtazamo wa Mwelekeo Lemevu. Mtazamo huu uliibuka katika miaka ya mwongo wa sabini. Tafiti za hapo awali zilidhihirisha kwamba mtazamo wa hapo awali wa Mwelekeo Punguani uliokuwa ukitumika wakati huo ulikuwa na upungufu mwingi na uliwadunisha wanawake.

Mtazamo wa Mwelekeo Lemevu unasisitiza kwamba tofauti au uweza wa kiisimu miongoni mwa wanawake na wanaume unatokana na misingi ya umenke ambapo wanaume hutawala ilhali wanawake hutawaliwa katika hali zote za kimaisha. Hivyo basi, waitifaki wa mtazamo huu wanasisitiza kuwa tofauti za kisutua miongoni mwa wanawake na wanaume, ndicho chanzo cha tofauti za umenke katika matumizi ya lugha.

Thorne na Henley (1975), Zimmerman na West (1975), Fishman (1983) pamoja na Thorne, Kramae na Henley (1983) ni baadhi ya watafiti ambao wametumia mtazamo

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

huu katika kuchunguza mazungumzo miongoni mwa wanawake na wanaume. Katika tafiti zao, watafiti hawa walitumia vigezo vya ukataji kauli na uanzishaji wa mada katika mazungumzo. Ilibainika kwamba wanaume walionekana kuwakata kauli wanawake mara kwa mara, hivyo basi kutawala mazungumzo. Hata miongoni mwa wagonjwa, West (1984) aligundua kwamba wagonjwa wa kiume waliwakata kauli mara kwa mara madaktari wa kike kuliko wale wa kiume. Jambo hili linadhihirisha kwamba wanawake hawapewi muda wa kujieleza hata wakati ambao ni muhimu kwao kujieleza au kuelezea kuhusu jambo muhimu kama vile kutibu mgonjwa!

Tumepata kichocheo cha kutumia mtazamo huu wa Mwelekeo Lemevu kwa sababu kiini cha utafiti huu ni kuchunguza na kubainisha nani anatawala mazungumzo ya darasani. Mtazamo huu huwasawiri wanawake kuwa viumbe wanaonyanyaswa katika hali zote za kimaisha. Aidha kwa mujibu wa mtazamo huu, tofauti zinazodhihirika za kiisimu kati ya wanaume na wanawake husababishwa na mahusiano ya kisutua ambapo wanaume wanaonekana kuwa wenye nguvu kuliko wanawake, hivyo basi, kutaka kuwatawala katika hali zote za kimaisha, mazungumzo yakiwemo.

Wanaoshikilia mtazamo huu wanasema kwamba, nafasi za kuzungumza, idadi ya maneno katika mazungumzo, kukatana kauli, ukimya na kadhalika ni baadhi ya vigezo vinavyotumika katika kupima utawalaji wa mazungumzo. Ninakisia kwamba hali ilivyo nchini Kenya ni kuwa hakuna usawa miongoni mwa wanawake na wanaume na huenda ikawa wanawake hawapewi nafasi za kujieleza katika hali mbalimbali za mazungumzo.

Katika Utafiti huu, tumetumia vigezo vya nafasi za uzungumzi na idadi ya maneno. Kwanza, kwa kutumia vigezo hivi tumeweza kubainisha ni nani wanaotawala mazungumzo darasani. Pili, tumeweza kujua majukumu ya wahusika katika mazungumzo hayo, jambo ambalo limetuwezesha kujua kiini cha hali ilivyo. Mwisho, tumeweza

kubainisha jinsi utaratibu unaotumika wa kupeana nafasi za kuzungumza unavyoathiri utawalaji wa mazungumzo.

2.5 Muhtasari

Katika sura hii, tumeona kwamba swala la utawalaji wa mazungumzo ya darasani miongoni mwa wasichana na wavulana wa shule za upili za mseto halikuwa limefanyiwa utafiti wa kina. Kwa hivyo, utafiti wetu huu ulilenga kuziba pengo hili na kutoa mchango zaidi kwa wasomi katika nyanja pana ya lugha na umenke, hususan, katika mazungumzo ya darasani, katika muktadha wa mazingara ya Kiafrika.

Ili kuweza kupata muelekeo, tumejaribu kuangalia kazi za watafiti walioshughulikia swala hili. Tumeona kuwa baadhi ya kazi nyingi za awali zilimulika tu nani wanatawala mazungumzo ya darasani pasi na kuchunguza jukumu la mwalimu na wanafunzi (wasichana na wavulana) katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani.

Katika utafiti wetu tulijaribu kuchunguza hali zote hizi, yaani, jukumu la mwalimu na wanafunzi katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani. Mwisho, katika sura hii tumezungumzia kuhusu nadharia ambayo imetuongoza katika utafiti huu. Kwa kifupi ni kuwa, sura hii imetusaidia sana hasa katika kujua kazi za awali ambazo zilifanywa kuhusu somo hili na hivyo basi kutuwezesha kujua mapengo ambayo yalikuwa hayajajazwa na kazi hizo za awali. Katika sura inayofuata, tumewasilisha na kutoa uchanganuzi wa data tuliyopata nyanjani.

SURA YA TATU

MATOKEO YA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Katika sura hii tunawasilisha data iliyopatikana nyanjani katika hali ya majedwali na maelezo. Katika kuwasilisha data yenyewe, tumeongozwa na madhumuni ya utafiti. Data inawasilishwa kwa kuzingatia masomo na madarasa tofauti tofauti yaliyotumika katika utafiti. Baadaye, data yote ya shule "A" inawasilishwa katika jedwali moja. Mtindo huo huo umetumika katika kuwasilisha na kuchanganua data ya shule "B". Mwisho kabisa, data ya shule zote mbili imewasilishwa katika jedwali moja na halafu kuchanganuliwa.

Sura hii imegawanywa katika sehemu tatu kuu. Katika sehemu ya kwanza, imejadiliwa na kuchunguzwa ni nani kati ya wasichana na wavulana wanatawala mazungumzo ya darasani. Katika kujua jambo hili, vigezo kama vile nafasi za kuzungumza, idadi ya maneno na wastani wa maneno kwa kila nafasi vimechunguzwa kwa undani.

Katika sehemu ya pili, majukumu ya wasichana, wavulana na walimu katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani yamechunguzwa na kubainishwa. Katika kufanikisha lengo hili, vigezo vilivyotumika ni kama vile; idadi ya wanaoinua mikono, kutoinua mikono na nafasi ambazo zilitolewa aidha kwa wasichana au wavulana lakini hazikutumika. Vigezo hivi vimetuwezesha kujua majukumu ya wasichana na wavulana katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani.

Katika kujua majukumu ya walimu, tumejaribu kuchunguza jinsi mwalimu alivyoteua wanafunzi pale ambapo hakuna mwanafunzi aliyeinua mkono. Pili, mwalimu alimteua nani wakati kulipokuwa na idadi sawa ya wasichana na wavulana walioinua mikono. Mwisho idadi ya nafasi ambazo mwalimu aliwapatia wasichana wakati kulipokuwa na idadi ndogo ya wasichana walioinua mikono ikilinganishwa na ile ya wavulana walioinua mikono. Au pale

ambapo kulikwa na idadi ndogo ya wavulana walioinua mikono ikilinganishwa na ile ya wasichana.

Katika sehemu ya tatu ya sura hii, tumechunguza utaratibu unaoibuka wa kuteua wanafunzi na kujaribu kubainisha iwapo utaratibu huo unaendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani.

3.1 Utawalaji wa mazungumzo ya darasani

3.1.1 Idadi ya nafasi za kuzungumza, (Shule "A")

Kipengele cha kwanza kilichotumika katika kujua nani wanatawala mazungumzo ya darasani, ni idadi ya nafasi ambazo kila kikundi (wasichana na wavulana) kilipewa. Jedwali la kwanza hapo chini, linatuonyesha jumla ya nafasi walizopata wasichana na wavulana kutokana na kuinua au kutoinua mikono katika masomo ya Kiswahili na Kiingereza. Vile vile, jedwali hili linatuonyesha idadi ya maneno iliyochangiwa na kila kikundi katika masomo hayo mawili. Aghalabu, jedwali hili pia linatuonyesha asilimia ya nafasi na asilimia ya maneno yaliyochangiwa na kila kikundi.

Jedwali – 1: Wanafunzi walivyochangia: shule "A" (Angalia kiambatisho – ix)

		Wavulana			**Wasichana**		
		Kiswahili	Kiingereza	**Jumla**	Kiswahili	Kiingereza	**Jumla**
Idadi ya nafasi	Kidato - 3	31	20	51	20	15	35
	Kidato - 4	19	14	33	11	8	19
	Jumla / Asilimia	**50 = 61.7%**	**34 = 59.6%**	**84 = 60.9%**	**31 = 38.3%**	**23 =40.4%**	**54=39.1%**
Idadi ya maneno	Kidato - 3	74	174	248	29	67	96
	Kidato - 4	65	87	152	29	28	57
	Jumla / Asilimia	**139 =70.6%**	**261 =73.3%**	**400 =72.3%**	**58 = 29.4%**	**95 =26.7%**	**153=27.7 %**

Kutokana na jedwali la kwanza (1) katika ukurasa wa ishirini na tano (25), katika somo la Kiswahili, Shule "A" wavulana walipewa jumla ya nafasi hamsini (50) ilhali wasichana wakapewa jumla ya nafasi thelathini na moja (31). Katika somo hili, inadhihirika waziwazi kuwa wavulana walipewa nafasi nyingi zaidi, hii ikiwa ni asilimia sitini na moja nukta saba (61.7%) ikilinganishwa na asilimia thelathini na nane nukta tatu (38.3%) ya nafasi walizopewa wasichana.

Katika somo la Kiingereza, Shule "A", jumla ya nafasi zote zilizotolewa zilikuwa hamsini na saba (57). Kati ya hizi, wavulana walipewa nafasi thelathini na nne (34) hii ikiwa ni asilimia hamsini na tisa nukta sita (59.6%) wasichana wakapewa nafasi ishirini na tatu hii ikiwakilisha asilimia arubaini nukta nne (40.4%) ya nafasi zote. Katika somo hili vile vile wavulana waliweza kupewa nafasi nyingi kuliko wasichana.

Kwa jumla katika Shule "A", wavulana walipewa jumla ya nafasi themanini na nne (84), hii ikiwakilisha asilimia sitini nukta tisa (60.9%), wasichana wakapewa jumla ya nafasi hamsini na nne (54), hii ikiwa ni asilimia thelathini na tisa nukta moja (39.1%). Inadhihirika waziwazi kuwa wavulana walipewa nafasi nyingi zaidi wakilinganishwa na wasichana.

3.1.2 Idadi ya maneno yaliyochangiwa (shule "A")

Kipengele cha pili kilichotumika katika kupima ni nani wanatawala mazungumzo ya darasani, ni idadi ya maneno iliyochangiwa na kila kikundi. Kama inavyodhihirika katika jedwali la kwanza (1), ukurasa wa ishirini na tano (25), wavulana katika somo la Kiswahili shule "A", walichangia maneno mia moja thelathini na tisa (139). Hii iliwakilisha asilimia sabini nukta sita (70.6%) na wasichana wakachangia maneno hamsini na nane pekee (58) ambapo hii inawakilisha asilimia ishirini na tisa nukta nne (29.4%). Hapa inabainika kuwa wavulana walichangia mara mbili zaidi ya wasichana.

Katika somo la Kiingereza, wavulana walichangia maneno mia mbili sitini na moja (261) hii ikiwa ni asilimia sabini na tatu nukta tatu (73.3%), wasichana kwa upande wao wakachangia maneno tisini na tano (95) tu! Hii ikiwa ni asilimia ishirini na sita nukta saba (26.7%) ya maneno yote. Hivyo, katika somo hili wavulana vile vile, walichangia zaidi ya mara mbili, zaidi ya wasichana.

Jumla ya maneno yote yaliyochangiwa na wanafunzi katika shule hii ni mia tano hamsini na tatu (553). Wavulana walichangia maneno mia nne (400) hii ikiwa ni asilimia sabini na mbili nukta tatu (72.3%) ilhali wasichana wakachangia maneno mia moja hamsini na tatu (153) hii ikiwakilisha asilimia ishirini na saba nukta saba (27.7%) pekee! Kwa jumla basi, wavulana katika shule hii walichangia maneno mengi kuliko wasichana.

3.1.3 Wastani wa maneno kwa kila nafasi (Shule "A")

Kipengele cha mwisho kilichotumika katika kujua ni kina nani wanatawala mazungumzo ya darasani ni kile cha wastani wa maneno kwa kila nafasi kwa wasichana na wavulana, na pia wastani uliohitajika kwa jumla katika masomo yote mawili. Katika kupata wastani huu, tumegawanya idadi ya meneno yaliyochangiwa na ile ya nafasi zilizopatikana kwa kila kikundi (wasichana na wavulana). Haya yanadhihirika katika jedwali la pili (2).

Jedwali – 2: Wastani wa maneno kwa kila nafasi (shule "A")

(Wv – Wavulana: Ws – Wasichana)

	Kiswahili			**Kiingereza**			**Jumla shule "A"**		
	Wv	**Ws**	**Jumla**	**Wv**	**Ws**	**Jumla**	**Wv**	**Ws**	**Jumla**
Idadi ya maneno	139	58	**197**	261	95	**356**	400	153	**553**
Idadi ya nafasi	50	31	**81**	34	23	**57**	84	54	**138**
Wastani	**2.8**	**1.9**	**2.4**	**7.7**	**4.1**	**6.2**	**4.8**	**2.8**	**4.0**

Kwa mujibu wa jedwali la pili (2) ukurasa wa ishirini na saba (27), tunaona kwamba katika somo la Kiswahili, jumla ya maneno ni mia moja tisini na saba (197). Idadi ya nafasi zote ni themanini na moja (81). Jumla ya wastani uliohitajika wa maneno kwa kila nafasi ulikuwa maneno mawili nukta nne (2.4). Inabainika kuwa wavulana walikuwa na wastani wa maneno mawili nukta nane (2.8) kwa kila nafasi hivyo kupitisha wastani uliohitajika wa maneno mawili nukta nne (2.4).

Wasichana hawakufikisha wastani uliohitajika wao walikuwa na wastani wa neno moja nukta tisa (1.9) kwa kila nafasi hii ikiwa chini ya wastani uliohitajika kwa kiwango cha nukta tano (0.5). Hivyo, mbali na kuwa na wastani mkubwa kuliko wasichana, wavulana vile vile waliweza kupitisha wastani uliohitajika wa maneno mawili nukta moja kwa kila nafasi.

Kama inavyodhihirika katika jedwali la pili (2), katika somo la Kiingereza, maneno yaliyochangiwa ni mia tatu hamsini na sita (356) ilhali nafasi zote ni hamsini na saba (57). Wastani wa maneno kwa kila nafasi uliohitajika ni maneno sita nukta mbili (6.2). Wavulana walikuwa na wastani wa maneno saba nukta saba (7.7) kwa kila nafasi hivyo kupitisha wastani uliohitajika kwa kiwango cha moja nukta tano.

Wasichana walikuwa na wastani wa maneno manne nukta moja (4.1) ambapo wastani huu ulikuwa chini ya wastani uliohitajika wa maneno sita nukta mbili (6.2) kwa kiwango cha maneno mawili nukta moja (2.1). Wavulana katika somo hili la Kiingereza, licha ya kuwa na wastani mkubwa wa maneno kwa kila nafasi, pia waliweza kupitisha wastani uliohitajika wa maneno sita nukta mbili (6.2) kwa kila nafasi.

Jumla ya nafasi zote walizopata wanafunzi katika shule "A" ni mia moja thelathini na nane (138). Jumla ya maneno yote ni mia tano hamsini na tatu (553). Wastani wa maneno kwa kila nafasi katika shule hii ni maneno manne nukta sufuri (4.0). Kwa mujibu wa jedwali la pili (2) ukurasa wa ishirini na saba (27), wavulana walikuwa na wastani wa maneno manne

nukta nane (4.8) kwa kila nafasi hivyo kupitisha wastani uliohitajika wa maneno manne nukta sufuri (4.0).

Wasichana hawakufikisha wastani uliohitajika wao walikuwa na wastani wa maneno mawili nukta nane (2.8) kwa kila nafasi, hii ikiwa chini ya wastani uliohitajika kwa kiwango cha neno moja nukta mbili (1.2).

Kwa muhtasari, katika shule "A" wavulana walipata nafasi nyingi zaidi, na kwa idadi ya maneno, walichangia mara mbili zaidi ya wasichana. Mbali na hivyo, wavulana ndio waliokuwa na, wastani mkubwa wa maneno kwa kila nafasi na pia walipitisha wastani uliohitajika wa maneno manne nukta sufuri (4.0) kwa kila nafasi.

Wasichana kwa upande wao, licha ya kupata nafasi kidogo, walichangia maneno machache wakilinganishwa na wavulana. Mbali na hivyo, walikuwa na wastani mdogo wa maneno kwa kila nafasi pia wastani wao wa maneno kwa kila nafasi haukufikia wastani kuliohitajika cha maneno manne nukta sufuri (4.0).

3.1.4 Idadi ya nafasi walizopata Shule "B"

Jedwali – 3: wanafunzi walivyochangia: shule "B" (Angalia kiambatisho - ix)

		Wavulana			Wasichana		
		Kiswahili	Kiingereza	**Jumla**	Kiswahili	Kiingereza	**Jumla**
Idadi ya nafasi	Kidato - 3	31	12	43	21	8	29
	Kidato - 4	7	15	22	7	11	18
	Jumla / Asilimia	**38 = 57.7%**	**27 = 58.7%**	**65 = 58%**	**28 = 42.4%**	**19 = 41.3%**	**47 = 42%**
Idadi ya maneno	Kidato - 3	89	64	248	36	67	41
	Kidato - 4	97	105	152	100	28	51
	Jumla / Asilimia	**186 = 57.8%**	**169 = 64.8%**	**355= 60.9%**	**136= 42.2%**	**95 = 35.2%**	**92 = 39.1%**

Kama inavyodhihirika katika jedwali la tatu (3) ukurasa wa ishirini na tisa (29), katika somo la Kiswahili shule "B", wavulana walipata jumla ya nafasi thelathini na nane (38). Idadi hii iliwakilisha asilimia hamsini na saba nukta sita (57.6%) na wasichana wakapata nafasi ishirini na nane (28) hii ikiwa ni asilimia aubaini na mbili nukta nne (42.4%). Wavulana hivyo walipata nafasi nyingi kuliko wasichana.

Katika somo la Kiingereza shule "B", wavulana walipata nafasi ishirini na saba (27), hii ikiwa ni asilimia hamsini na nane nukta saba (58.7%). Wasichana wakapata nafasi kumi na tisa (19) hii ikiwakilisha asilimia arubaini na moja nukta tatu (41.3%). Inabainika kuwa wavulana vile vile katika somo hili walipata nafasi nyingi kuliko wasichana.

Kwa jumla katika Shule "B", kati ya nafasi mia moja kumi na mbili (112) zilizotolewa, wavulana walipata jumla ya nafasi sitini na tano (65), hii ikiwa ni asilimia hamsini na nane (58%). Wasichana nao wakapata nafasi arubaini na saba (47) hii ikiwa ni asilimia arubaini na mbili (42%) ya nafasi zote. Hivyo kwa jumla ni kuwa katika shule "B" wavulana walipata nafasi nyingi kuliko wasichana.

3.1.5 Idadi ya maneno yaliyochangiwa shule "B"

Katika idadi ya maneno, wavulana katika somo la Kiswahili walichangia maneno mia moja themanini na sita (186) hii ikiwa ni asilimia hamsini na saba nukta nane (57.8%) na wasichana wakachangia maneno mia moja thelathini na sita hii ikiwakilisha asilimia arubaini na mbili nukta mbili (42.2%) ya maneno yote. Wavulana hivyo walichangia maneno mengi kuliko wasichana.

Katika somo la Kiingereza, kama inavyodhihirika katika jedwali la tatu (3) ukurasa wa ishirini na tisa (29), wavulana walichangia maneno mia moja sitini na tisa (169), ambapo hii

iliwakilisha asilimia sitini na nne nukta nane (64.8%). Wasichana walichangia maneno tisini na mbili (92), hii ikiwa ni asilimia thelathini na tano nukta mbili (35.2%). Wavulana basi waliweza kuchangia karibu mara mbili zaidi ya wasichana.

Kwa jumla katika shule hii, wavulana walichangia maneno mengi zaidi kuliko wasichana. Jumla ya maneno yote yaliyochangiwa na wanafunzi katika shule hii ni maneno mia tano themanini na tatu (583) (angalia jedwali 3, ukurasa wa 29). Kati ya maneno haya, Wavulana walichangia maneno mia tatu hamsini na tano (355) hii ikiwa ni asilimia sitini nukta tisa (60.9%). Wasichana nao wakachangia maneno mia mbili ishirini na nane (228) hii ikiwa ni asilimia thelathini na tisa nukta moja (39.1%).

3.1.6 Wastani wa maneno kwa kila nafasi shule "B"

Jedwali – 4: Wastani wa maneno kwa kila nafasi
Wv – Wavulana: Ws – Wasichana

	Kiswahili			**Kiingereza**			**Jumla shule "B"**		
	Wv	**Ws**	**Jumla**	**Wv**	**Ws**	**Jumla**	**Wv**	**Ws**	**Jumla**
Idadi ya maneno	186	136	**322**	169	92	**261**	355	228	**583**
Idadi ya nafasi	38	28	**66**	27	19	**46**	65	47	**112**
Wastani	**4.9**	**4.9**	**4.9**	**6.3**	**4.8**	**5.7**	**5.5**	**4.9**	**5.2**

Jumla ya nafasi zote zilizotolewa katika somo la Kiswahili kama inavyodhihirika katika jedwali la nne (4) hapo juu, ni sitini na sita (66). Idadi ya maneno yote ni mia tatu ishirini na mbili (322). Kutokana na tarakwimu hizo, wastani wa maneno kwa kila nafasi ni maneno manne nukta tisa (4.9). Makundi yote mawili yaani wasichana na wavulana, yaliweza kufikisha wastani huu kwani wote walikuwa na wastani wa maneno manne nukta tisa (4.9) kwa kila nafasi. Inadhihirika kuwa katika somo la Kiswahili, wasichana na wavulana waliweza

kupata wastani sawa wa maneno kwa kila nafasi. Hii inatokana na hali kuwa waliweza kupata idadi sawa ya nafasi na kuchangia maneno sawa kwa sawa katika kidato cha nne. Tunakisia kuwa hali hii ya wasichana na wavulana kuweza kuchangia sawa kwa sawa katika mazungumzo, katika smo hili, ilitokana na hali kuwa huenda ikawa mwalimu alielewa umuhimu wa kuwapatia wasichana na wavulana nafasi sawa za kuzungumzoa Hii ni kwa sababu ni mwalimu ndiye aliyesababisha kwa hali hii kutokea kutokana na jinsi alivyokuwa akiwapatia wanafunzi nafasi za kuzungumza.

Katika somo la Kiingereza, idadi ya maneno yaliyochangiwa ni mia mbili sitini na moja, (261) ilhali nafasi zote katika somo hili zilikuwa arubaini na sita (46). Wastani wa maneno ulihitajika kuwa maneno matano nukta saba (5.7) kwa kila nafasi. Wavulana walipitisha wastani huu kwa kwa kiwango cha nukta sita (0.6) kwani walikuwa na wastani wa maneno sita nukta tatu (6.3) kwa kila nafasi. Wasichana hawakufikisha wastani uliohitajika. Wao walikuwa na wastani wa maneno manne nukta nane (4.8) kwa kila nafasi.

Kwa jumla, nafasi zote walizopata wanafunzi katika shule "B" ni mia moja kumi na mbili (112). Jumla ya maneno yote ni mia tano themanini na tatu (583). Wastani uliohitajika wa maneno kwa kila nafasi katika shule hii ni maneno matano nukta mbili (5.2). Kwa mujibu wa jedwali la nne (4) ukurasa wa thelathini na moja (31), wavulana walikuwa na wastani wa maneno matano nukta tanoi (5.5) kwa kila nafasi hivyo kupitisha wastani uliohitajika wa maneno matano nukta mbilii (5.2). Wasichana hawakufikisha wastani uliohitajika wao walikuwa na wastani wa maneno manne nukta tisa (4.9) kwa kila nafasi, hii ikiwa chini ya wastani uliohitajika kwa kiwango cha nukta tatu (0.3).

Kwa ufupi, shule "B", wavulana ndio waliopata nafasi nyingi na pia kuchangia maneno mengi kuliko wasichana. Mbali na kuwa na wastani mkubwa wa maneno kwa kila

nafasi wavulana walipitisha kiwango cha wastani uliohitajika wa maneno matano nukta mbili (5.2) kwa kila nafasi.

Wasichana walipata nafasi chache za kuzungumza na walichangia maneno machache wakilinganishwa na wavulana. Pia, walikuwa na wastani mdogo wa maneno kwa kila nafasi, na licha ya hivyo, hawakufikisha wastani uliohitajika wa maneno matano nuta mbili (5.2) kwa kila nafasi.

3.1.7 Shule "A" na Shule "B"

Jedwali – 5: Walivyochangia (shule "A" na "B")

	Idadi ya nafasi		**Idadi ya maneno**	
	Wavulana	Wasichana	Wavulana	Wasichana
A	84	54	400	153
B	65	47	355	228
Jumla/ Asilimia	**149 = 59.6%**	**101 = 40.4%**	**755 = 66.5%**	**381 = 33.5%**

Kwa jumla matokeo katika utafiti huu ni kuwa, wavulana walipata nafasi mia moja arubaini na tisa (149) hii ikiwa ni asilimia hamsini na tisa nukta sita (59.6%) ilahali wasichana wakaibuka na nafasi mia moja na moja (101) hii ikiwakilisha asilimia arubaini nukta nne (40.4%) ya nafasi zilizotolewa.

Katika idadi ya maneno, wavulana walichangia jumla ya maneno mia saba hamsini na tano (755), hii ikiwa ni asilimia sitini na sita nukta tano (66.5%) ya maneno yote. Kadhalika, wasichana walichangia maneno mia tatu themanini na moja (381), hii ikiwakilisha asilimia thelathini na tatu nukta tano (33.5%) ya maneno yote. Wavulana, hivyo walipata nafasi nyingi na pia walichangia maneno mengi kuliko wasichana.

Jedwali – 6: Wastani wa maneno kwa kila nafasi kwa jumla (Shule "A" na "B")

Wanafunzi	Idadi ya nafasi	Idadi ya maneno	Wastani wa maneno kwa nafasi
Wavulana	755	149	5.1
Wasichana	381	101	3.8
Jumla	**1136**	**250**	**4.5**

Kutokana na tarakwimu katika jedwali la sita (6) ukurasa wa thelethini na nne (34), wavulana walikuwa na wastani wa maneno matano nukta moja (5.1) kwa kila nafasi, ilhali wasichana wakawa na wastani wa maneno matatu nukta nane (3.8) kwa kila nafasi. Hivyo wavulana walipitisha wastani uliohitajika wa maneno manne nukta tano (4.5) kwa kila nafasi ilhali wasichana hawakufikisha wastani huu.

Kwa muhtasari, utafiti huu, licha ya kupata nafasi nyingi, wavulana vile vile walichangia idadi kubwa ya maneno wakilinganishwa na wasichana. Waliweza kuchangia mara mbili zaidi ya wasichana. Wavulana vile vile walikuwa na wastani mkubwa wa maneno kwa kila nafasi na pia walipitisha wastani uliohitajika wa maneno manne nuta tano (4.5).

Wasichana walipata nafasi chache, walichangia maneno kidogo, walikuwa na wastani mdogo wa maneno kwa kila nafasi na pia hawakufikisha wastani uliohitajika wa maneno manne nukta tano (4.5) kwa kila nafasi.

Mtazamo Mwelekeo Lemevu, unasisitiza kuwa nafasi za kuzungumza, idadi ya maneno, wastani wa maneno kwa kila nafasi, uanzishaji wa mada, na ukataji kauli ndio vigezo muhimu vinavyotumiwa katika kupima utawalaji wa mazungumzo. Kwa mujibu wa mtazamo huu, wale wanaokuwa na nafasi nyingi katika mazungumzo, kuchangia maneno mengi, kuwa na wastani mkubwa wa maneno kwa kila nafasi na kukata wenzao kauli mara

kwa mara katika mazungumzo ndio wanaotawala mazungumzo. Katika utafiti huu, kama nilivyosema hapo awali, tumetumia vigezo vya idadi ya nafasi za kuzungumza, idadi ya maneno, na wastani wa maneno kwa kila nafasi katika kujua ni nani, kati ya wavulana na wasichana wanatawala mazungumzo ya darasani.

Kwa kutumia vigezo nilivyovitaja hapo mbeleni, matokeo ya utafiti huu, yamebainisha kuwa wavulana ndio wanaotawala mazungumzo ya darasani. Tukizingatia kigezo cha nafasi za kuzungumza, katika shule "A," hii ikiwa ni shule ya kijijini, tunaona wavulana walipata nafasi nyingi kuliko wasichana. Kati ya nafasi mia moja thelathini na nane (138) zilizotolewa, wavulana walipata nafasi themanini na nne (84). Hii iliwakilisha asilimia sitini nukta tisa (60.9%) ya nafasi zote. Wasichana waliweza kupata nafasi hamsini na nne (54) pekee! Hii ikiwa ni asilimia thelathini na tisa nukta moja (39.1%).

Wavulana vile vile, ndio waliochangia idadi kubwa ya maneno wakilinganishwa na wasichana. Wavulana walichangia maneno mia nne (400) ilhali wasichana wakachangia maneno mia moja na hamsini na tatu pekee (153). Hivyo, wavulana walichangia zaidi ya mara mbili ya wasichana. Mbali na hayo, wavulana waliweza kupitisha wastani uliohitajika wa maneno manne nukta sufuri (4.0) kwa kila nafasi ilhali wasichana hawakufikisha wastani huo.

Mambo hayakuwa tofauti katika shule "B", hii ikiwa ni shule ya mjini. Katika shule hii, wavulana walipata nafasi nyingi za kuzungumza kuliko wasichana, walichangia maneno mengi zaidi na pia kuwa na wastani mkubwa wa maneno kwa kila nafasi wakilinganishwa na wasichana.

Kwa jumla, kama ilivyobainika katika jedwali la sita (6), ukurasa wa thelathini na nne (34), ni kuwa wavulana walipata nafasi nyingi zaidi, walichangia maneno mengi zaidi na pia kuwa na wastani mkubwa wa maneno kwa kila nafasi. Kwa jumla wavulana walipata nafasi mia moja arubaini na tisa (149) hii ikiwakilisha asilimia hamsini na tisa nukta sita (59.6%).

Pili wavulana walichangia jumla ya maneno mia saba hamsini na tano (755), hii ikiwa ni mara mbili zaidi ya maneno yaliyochangiwa na wasichana (asilimia sitini na sita nukta tano). Mwisho, mbali na kuwa na wastani mkubwa wa maneno matano nukta moja (5.1) kwa kila nafasi, waliweza kupitisha wastani uliohitajika wa maneno manne nukta tano (4.5)

Wasichana kwa upande wao walipata nafasi mia moja na moja (101) hii ikiwakilisha asilimia arubaini nukta nne (40.4%) pekee ya nafasi zote. Pili, walichangia maneno machache:- mia tatu themanini na moja (381) hii ikiwa ni asilimia thelathini na tatu nukta tano (33.5%) tu. Mwisho, mbali na kuwa na wastani mdogo wa maneno matatu nukta nane (3.8) kwa kila nafasi, hawakufikisha wastani uliohitajika wa maneno manne nukta tano (4.5) kwa kila nafasi.

Kutokana na hali hii ya kutochangia ipasavyo katika mazungumzo ya darasani, ni dhahiri kuwa wasichana wanatawaliwa katika mazungumzo hayo. Jambo hili mara nyingi huathiri uelewa wao kwani mazungumzo, imebainika ni kifaa muhimu sana katika kuelewa maswala mbalimbali. Iwapo wasichana hawatahusishwa ipasavyo katika mazungumzo ya darasani, basi huenda hali hii ikawaathiri katika masomo yao na jinsi watakavyohusiana na wanajamii kwa jumla.

Ingawaje, kwa jumla wavulana walitawala mazungumzo ya darasani, hali haikuwa hivyo katika somo la Kiswahili, kidato cha nne, shule "B" (shule ya mjini). Katika somo hili, kati ya nafasi kumi na nne (14) zilizotolewa, wavulana walipata nafasi saba (7) na wasichana vilevile wakapata nafasi saba (7). Vile vile katika idadi ya maneno, wote waliweza kuchangia karibu idadi sawa ya maneno. Wavulana walichangia maneno tisaini na saba (97) hii ikiwakilisha asilimia arubaini na tisa nukta mbili (49.2%) na wasichana wakachangia maneno mia moja (100), hii ikiwa ni asilimia hamsini nukta nane (50.8%). (Angalia jedwali 3 ukurasa wa 29 na pia ix ukurasa wa 64).

Katika kuchunguza zaidi kwa nini hali ilikuwa hivi, ilibainika kuwa hali ilikuwa hivyo kwa sababu mwalimu alionekana kuelewa umuhimu wa kuwapatia wasichana na wavulana nafasi za kuzungumza. Hii ilidhihirika kwa jinsi alivyokuwa akiteua wanafaunzi darasani. Kila alipomteua mvulana kuzungumza, swali lililofuatia alimteua msichana (soma kiambatisho xi ukurasa wa 66). Hali hii iliendelea hivyo mpaka mwisho wa somo. Kufikia mwisho wa somo, kutokana na kuinua mikono, mwalimu alikuwa ameteua wavulana sita (6) na wasichana sita (6). Wale walioteuliwa bila ya kuinia mikono walikuwa mvulana mmoja (1) na msichana mmoja (1). (Angalia kiambatisho vii uk. 62). Tunaona kuwa hali hii haikutokana na sababu kuwa shule hii iko mjini bali ni kwa sababu mwalimu alionekana ksisitiza kuwa wasichana na wavulana wapate nafasi sawa katika mazungumzo.

Kwa mfano hivi ndiyo mambo yalivyokuwa;

MAELEZO:
Msisitizo katika mabano – maelezo au idadi ya wanaoinua mikono
Msisitizo na mlazo – majibu ya wanafunzi yatakayotumika katika uchanganuzi.
Ms – Msichana: **Ws** – wasichana: **Mv** – mvulana: **Wv** – Wavulana
Ach. –Achaguliwa

Unasaji ulianza mwanzo wa somo

1. **Mwalimu**: Leo tuna mgeni ambaye ametutembelea na atakuwa na sisi darasani na kuangalia jinsi tunavyosoma.... (**Baada ya kusoma anauliza maswali**) Makala hayo yanahusu nini? (**Ws - 3: Wv -3: Ach. Mv**)
   Mv: Makala haya yanahusu sayansi ya kutumbisha

2. **Mwalimu**: Vyema, Sayansi ya Kutumbisha. Kwa hivyo, sayansi ya kutumbisha na madhara yake ndio inayoelezwa hapa...(**Wanasoma maswali tena**) Inua mkono unipe jibu la swali la kwanza. Andika kichwa kifaacho cha makala hii (**Ws - 4:Wv -2 : Ach. Ms**)
   Ms: Kichwa kifaacho cha makala hii ni sayansi ya kutumbisha.

3. **Mwalimu**:..Swala la sayansi ya kutumbisha linaweza kumsaidia binadamu mabaa gani mawili yanayotukabili sasa? Swali hili nampa mvulana si lazima * wale ambao wameinua mikono hata wale ambao hawakuinua. (**Ws –0:Wv –3**) Wewe hapo (**Ach. Mv**)
   Mv: Itaondoa janga la kiangazi

4. **Mwalimu**: Mwingine atwambie baa la pili? (**Ws - 2: Wv -0**) Msichana sasa (**Ach. Ms**)*
   Ms: ***Itaondoa uhaba wa mashamba***

5. **Mwalimu** Kila mmoja nitampatia nafasi atoe maoni yake*. Swali linasema unadhani ni kwa nini wanyama waliozalishwa kutumia sayansi hii bado wako mahabarani? Kila mmoja nitampatia nafasi, mvulana, msichana, mvulana msichana. Aliye tayari ni nani? (**Ws -3 :Wv -2**) Haya anza (**Ach. Mv**)
   Mv: ***Wanyama wengi waliozalishwa kwa kutumia sayansi hii ni wadogo wadogo hivyo basi huhifadhiwa katika mahabara ili kuendeleza mbele utafiti.***

6. **Mwalimu**: Hatuwezi kuwatumia kwa chakula (**Ws - 0: Wv -2: Ach. Mv**)
   Mv: ***Hatuwezi mwalimu.***

7. **Mwalimu** Hilo ni wazo zuri sana...tupate msichana* sasa tupate mawazo yake. (**Ws - 3:Wv - 0:**) Gladys? (**Ach. Ms**) Unadhani ni kwa nini wanyama waliozalishwa kwa kutumia sayansi hii ya kutumbisha bado wangali mahabarani?
   Ms: ***Mimi naona kama ambaye yani bado wako kule kwenye mahabara kwa sababu wale wanasayansi bado wanafanya utafiti zaidi kulingana na vile wale wanyama kama kwa kweli wanaweza kuwa wakubwa***
   (Kiambatisho cha xi Uk – 66)

Hali hii ya uteuzi wa msichana – mvulana, ndio iliyowezesha wasichana na wavulana kupata nafasi sawa za kuzungumza na pia kuchangia idadi sawa ya maneno katika mazungmzo. Jambo hili linadhihirisha kuwa upo uwezekano wa wasichana na wavulana kuhusishwa kikamilifu katika mazungumzo ya darasani pasi kikundi kimoja kuonekana kutawala mazunguzo hayo. Hatukuweza kubainisha iliwezekanaje kwa mwalimu kuwapa wanafunzi nafasi sawa za kuzungumza. Ni makisio yetu kuwa huenda ikawa mwalimu alielewa umuhimu wa kuwapatia wanafunzi nafasi sawa za kuzungumza darasani. Hata hivyo, jambo hili linahitaji utafiti zaidi. Hali hii ilikuwa kinyume na masomo mengine ambapo mwalimu alionekana wakati mwengine kuteua wavulana hata zaidi ya wawili bila kuteua msichana. Kwa mfano katika somo la Kiingereza kidato cha tatu shule "A".

Hivi ndivyo ilivyokuwa:

1. **Mwalimu**: Next? *(Mwingine?)* (**Ws – 5: Wv – 8 Mv Acha.**)
   Mv: ***Wamala***

2. **Mwalimu**: Another one? *(Muhusika mwingine?)* **(Ws –5: Wv – 4: Ms Acha.)**
   Ms: ***Kaija***
3. **Mwalimu**: Another character? *(Muhusika mwengine?)*
   (Ws – 5: Wv – 4: Mv achaguliwa)
   Mv: ***Nyakake***
4. **Mwalimu**: Yes, another character? *(Sawa muhusika mwengine?)*
   (Ws – 5: Wv – 3:achaguliwa Mv ambaye hakunyosha mkono)
   Mv: ***Vincent***
5. **Mwalimu**: Next? *(Mwingine?)* **(Ws – 1: Wv – 0: Ach. Mv ambaye hakunyosha mkono)**
   Mv: ***Yankees***
6. **Mwalimu**: Another character? *(Muhusika mwingine?)* **(Ws – 0: Wv – 6: Mv achaguliwa)**
   Mv: ***Yankees secretary***
   (Kambatisho xii uk – 71)

Hapa tunaona kuwa mwalimu aliteua wavulana wanne mfululizo bila ya kuteua msichana.

3.2 Majukumu ya wahusika katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo.

Katika kuendeleza utwalaji wa mazungumzo ya darasani, wahusika, (mwalimu wasichana na wavulana) wana majukumu fulani. Kuna mambo yanayodhihirika ambayo husababisha kikundi fulani kutawala mazungumzo ilhali kikundi kingine kuonekena kutochangia ipasavyo. Katika kuangalia majukumu ya wanafunzi, tulichunguza na kuhesabu ni mara ngapi wasichana waliinua mikono, ni mara ngapi wavulana waliinua mikono, ni mara ngapi hawakuinua mikono, na mwisho, nafasi ambazo wasichana na wavulana walipewa lakini hawakuzitumia.

Katika kubainisha jukumu la mwalimu, tulichunguza jinsi mwalimu alivyoteua wanafunzi wakati ambapo hakukuwa na mwanafunzi aliyeinua mkono. Pili mwalimu alimteua nani pale ambapo kulikuwa na idadi sawa ya wasichana na wavulana walioinua mikono. Mwisho, tumechunguza na kuhesabu ni mara ngapi mwalimu aliteua wasichana wakati kulipokuwa na idadi ndogo ya wasichana kuliko ile ya wavulana walioinua mikono, na ni

mara ngapi aliteua wavulana wakati kulipokuwa na idadi ndogo ya wavulana kuliko ile ya wasichana waliokuwa wameinua mikono.

3.2.1 Majukumu ya wasichana na wavulana katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani.

Imebainika kwamba wanafunzi (wavulana na wasichana) wana majukumu fulani katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani. Kuna tabia fulani ambazo huenda zinasababisha wavulana kutawala au wasichana kutawaliwa katika mazungumzo ya darasani.

Zimmerman na West (ibid) wanasema kuwa wanawake hutumia muda wao mwigi kusikiliza na wala sio kuzungumza. Wanaendelea kusema kwamba huenda ikawa wasichana huiga tabia hii kutoka nyumbani na kuileta shuleni ikawa kwamba hawashiriki kikamilifu katika mazungumzo ya darasani jambo ambalo husababisha wao kutawaliwa katika mazungumzo.

Jedwali – 7: Jinsi walivyoinua mikono na kutumia nafasi walizopata

	Mara walizoinua mikono		**Mara wasizoinua mikono**		**Nafasi walizopata lakini hawakuzitumia**	
	Wavulana	Wasichana	Wavulana	Wasichana	Wavulana	Wasichana
Shule "A"	100	81	38	57	2	7
Shule "B"	79	64	25	40	2	5
Jumla	**179**	**145**	**63**	**97**	**4**	**12**

Katika utafiti huu imebainika kuwa wasichana kwa kiasi kikubwa walichangia sana katika utawalaji wa mazungumzo dhidi yao. Katika kuzingatia kipengele kile cha uinuaji wa

mikono, inadhihirika kuwa, katika shule "A", wavulana waliinua mikono mara nyingi zaidi kuliko wasichana. Wavulana waliinua mikono mara mia moja (100) hii ikiwa ni asilimia hamsini na tano nukta mbili (55.2%), ilhali wasichana wakainua mara themanini na moja (81) hii ikwakilisha asilimia arubaini na nne nukta nane (44.8%) ya mara zote ambazo mikono iliinuliwa. (Angalia jedwali 7 hapo juu)

Katika shule "B", vile vile tunaona wavulana ndio walioinua mikono mara nyingi. Wavulana waliinua mikono mara sabini na tisa (79) ilhali wasichana wakainua mara sitini na nne (64). Kwa jumla katika utafiti huu wavulana waliinua mikono mara mia moja sabini na tisa (179), hii iliwakilisha asilimia hamsini na tano nukta mbili (55.2%). Wasichana nao waliinua mikono mara mia moja arubaini na tano (145) hii ikiwa ni asilimia arubaini na nne nukta nane (44.8%) ya mara zote ambazo mikono iliinuliwa.

Kwa kutumia kigezo hiki cha uinuaji wa mikono, inaonekana wazi wazi kuwa wavulana, kwa kuinua mikono mara nyingi waliweza kuwa na uwezekano mkubwa wa kuteuliwa, na hivyo, kupata nafasi nyingi. Wasichana kwa upande wao, hawakuinua mikono mara nyingi na hivyo uwezekano, wa wao kuteuliwa ulikuwa mdogo, jambo ambalo huenda lilisababisha wao kupata nafasi chache za kuzungumza.

Kigezo hiki kinaenda sambamba na kigezo kile cha kutoinua mikono. Inadhihirika kuwa ni mara chache tu, ambazo wavulana hawakuinua mikono, ikilinganishwa na mara ambazo wasichana hawakuinua mikono. Tunaona kuwa, wavulana hawakuinua mikono mara sitini na tatu (63) na wasichana hawakuinua mara tisaini na saba (97). Kwa kutoinua mikono mara kwa mara wasichana walijipunguzia uwezekano, wa wao kuteuliwa kuzungumza darasani na hivyo kupata nafasi kidogo. Jambo hili, lilisababisha wao kutawaliwa katika mazungumzo ya darasani.

Jambo la kushangaza ni kuwa wasichana mara nyingine hawakuinua mikono hata pale ambapo walionekana kujua majibu ya maswali waliyoulizwa. Jambo hili liliweza kubainika wakati mwalimu alipoteua msichana miongoni mwa wale ambao hawakuwa wameinua mikono. Msichana aliyeteuliwa aliweza kujibu swali lililokuwa limeulizwa.

Mwisho, imebainika kuwa hata walipopewa nafasi za kuzungumza, wasichana mara nyingi hawakuzitumia nafasi hizo vilivyo, ikilinganishwa na jinsi wavulana walivyotumia nafasi zao. Jambo hili lilisababisha wasichana kuchangia maneno machache tu wakilinganishwa na wavulana, ambao walitumia nyingi ya nafasi walizopewa, na hivyo kuchangia maneno mengi.

Kama inavyodhihirika katika jedwali la saba (7) ukurasa wa aubaini (40), katika shule "A", wasichana, kati ya nafasi walizopata, walikosa kutumia nafasi saba (7). Hii inamaanisha kuwa kati ya nafasi hamsini na nne (54) walizopewa, walikosa kutumia asilimia kumi na tatu (13%) ya nafasi zao. Wavulana nao, kati ya nafasi themanini na nne (84) walizopewa ni mbili (2) tu ambazo walikosa kuzitumia hii ikiwa ni asilimia mbili nukta nne (2.4%) pekee.

Katika shule "B", wasichana, kati ya nafasi arubaini na saba (47) walizopewa, tano (5) kati ya nafasi hizi hawakuzitumia. Wavulana kwa upande wao kati ya nafasi sitini na tano (65) walizopewa, ni nafasi mbili (2) tu ambazo hawakuzitumia. Kwa jumla tunaona kuwa wasichana walipewa nafasi mia moja na moja (101). Kati ya hizi, walikosa kutumia nafasi kumi na mbili (12) hii ikiwa ni asilimia kumi na moja nukta tisa (11.9%). Wavulana, kati ya nafasi mia moja arubaini na tisa (149) walizopewa, ni nafasi nne (4) tu ambazo hawakuzitumia hii ikiwa ni asilimia ndogo ya mbili nukta saba (2.7%).

Kwa kutotumia nafasi zao, wasichana walichangia maneno machache, jambo lililosababisha wao kuwa na wastani mdogo wa maneno kwa kila nafasi, wakilinganishwa na wavulana. Wavulana kwa upande wao, walitumia nafasi zao kwa wingi na hivyo basi

kuchangia maneno mengi zaidi. Jambo hili, lilisababisha wao kuwa na wastani mkubwa wa maneno kwa kila nafasi.

Jambo muhimu linalojitokeza ni kuwa wasichana na wavulana kwa kiasi fulani wanachangia katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani. Kwa kutoinua mikono kwa wingi na kutotumia nafasi zao kikamilifu, wasichana hawachangii ipasavyo katika mazungumzo. Jambo hili linasababisha wao kutawaliwa katika mazungumzo ya darasani. Wavulana kwa upande wao, kutokana na kuinua mikono kwa wingi, wanapata nafasi nyingi za kuzungumza na hivyo kuchangia zaidi katika mazungumzo. Mathalan, kutokana na uwezo wao wa kutumia ipasavyo nafasi wanazopewa, wavulana wanakuwa na nafasi nzuri ya kuchangia zaidi katika mazungumzo na hivyo basi kutawala mazungumzo ya darasani.

3.2.2 Jukumu la mwalimu katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo.

Jedwali – 8: Jinsi mwalimu alivyoteua wanafunzi

	Nafasi alizotoa wakati hakuna aliyeinua mkono		**Nafasi alizotoa kulipokuwa na idadi sawa ya walioinua mikono**		**Nafasi alizotoa kulipokuwa na idadi ndogo ya walioinua mikono**	
	Wavulana	Wasichana	Wavulana	Wasichana	Wavulana	Wasichana
Shule "A"	23	17	9	2	19	9
Shule "B"	16	16	6	4	18	9
Jumla	**39**	**33**	**15**	**6**	**37**	**18**

Utafiti huu umethibitisha kuwa mwalimu ana jukumu muhimu sana katika kuendeleza au kutoendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani. Kwa mujibu wa Spender (ibid), anasema kuwa iwapo kikundi fulani kinatawala mazungumzo ya darasani, basi kinafanya hivyo kutokana na usaidizi wa mwalimu. Hata hivyo tafiti za awali zimethibitisha kuwa mara nyigi walimu hawa huwa wanafanya hivyo bila kukusudia.

Katika kujua jukumu la mwalimu katika kuendeleza au kutoendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani, tulitumia vigezo vifuatavyo: kwanza kabisa, tulichunguza jinsi mwalimu alivyoteua wanafunzi pale ambapo hakukuwa na mwanafunzi hata mmoja aliyeinua mkono. Je, katika hali hii, mwalimu aliteua msichana au mvulana? Je, aliteua wasichana mara ngapi na wavulana mara ngapi?

Pili, tulichunguza jinsi mwalimu alivyotoa nafasi za kuzungumza pale ambapo kulikuwa na idadi sawa ya wavulana na wasichana waliokuwa wameinua mikono. Je, katika hali hii, mwalimu aliwapatia wasichana nafasi ngapi, na wavulana akawapa nafasi ngapi? Mwisho imebainika kuwa, kuna wakati ambapo mwalimu, aidha alimpatia msichana nafasi ya kuzungumza ingawaje kulikuwa na idadi ndogo ya wasichana waliokuwa wameinua mikono ikilinganishwa na ile ya wavulana. Pia, kuna wakati ambapo mwalimu alimpatia mvulana nafasi ya kuzungumza, ilhali ni wavulana wachache tu waliokuwa wameinua mikono yao wakilinganishwa na wasichana. Katika hali hii tumehesabu nafasi alizowapatia wasichana na zile alizowapatia wavulana.

Utafiti huu umebainisha kuwa, bila ya kuinua mikono, mwalimu aliwapatia wavulana nafasi nyingi kuliko alivyowapatia wasichana. Kwa mfano katika shule "A", nafasi walizopewa wavulana bila hata ya kuinua mikono zilikuwa ishirini na tatu (23), ikiwa hii, ni asilimia hamsini na saba nukta tano (57.5%) zikilinganishwa na nafasi kumi na saba (17) alizowapatia wasichana hii ikiwa ni asilimia arubaini na mbili nukta tano (42.5%) (angalia

jedwali 8 ukurasa 43). Mwalimu ndiye aliyekuwa na uwezo wa kuteua aidha msichana au mvulana, pale ambapo wote (wasichana na wavulana) walikuwa na uwezo au nafasi sawa ya kuteuliwa. Tarakwimu hizi, zinatuelekeza kuamini kuwa mwalimu, kwa kiasi fulani aliwapendelea wavulana, na hivyo basi kuwasaidia katika kupata nafasi nyingi, jambo ambalo lilisababisha wao kutawala mazungumzo ya darasani.

Katika shule "B" kama inavyodhihirika katika jedwali la nane (8) ukurasa wa arubaini na tatu (43), mambo yalikuwa tofauti kidogo. Hapa tunaona kuwa walimu waliweza kugawa nafasi hizi sawa kwa sawa kwani, kati ya nafasi thelathini na mbili (32) ambazo walizitoa pasi na kuinua mikono, walimu waliweza kuwapatia wasichana nafasi kumi na sita (16) na wavulana vile vile nafasi kumi na sita (16). Hata hivyo tunapochanganya matokeo haya inadhihirika kuwa wavulana walipewa nafasi nyingi kuliko wasichana. Kwa jumla walimu waliwapa wavulana nafasi thelathini na tisa (39) hii ikiwa ni asilimia hamsini na nne nukta mbili (54.2%) ilhali wasichana wakapewa nafasi thelathini na tatu (33) hii ikiwakilisha asilimia arubaini na saba nukta nane (45.8%).

Pili, katika kuchunguza jinsi mwalimu alivyoteua wanafunzi pale ambapo kulikuwa na idadi sawa ya wasichana na wavulana walio kuwa wameinua mikono, tumebainisha pia kuwa walimu waliwateua zaidi wavulana kuliko walivyowateua wasichana. Kwa mfano, katika shule "A", walimu waliwateua wavulana mara tisa (9) hii ikiwa ni asilimia themanini na moja nukta nane (81.8%) ikilinganishwa na mara mbili pekee (2) ambazo wasichana waliteuliwa, hii ikiwa ni asilimia kumi na nane nukta mbili pekee (18.2%)! Hivyo, tunaona kuwa ingawa wote (wasichana na wavulana) walikuwa uwezo sawa wa kuteuliwa, walimu waliwateua wavulana mara nyingi kuliko walivyowateua wasichana wasichana

Katika shule ya pili ("B"), walimu vile vile walionekana kuwasaidia zaidi wavulana. Kwa mfano, kama inavyodhihirika katika jedwali 8 ukurasa wa 43, wavulana waliteuliwa

mara sita (6) ilhali wasichana wakateuliwa mara nne. Hivyo asilimia sitini (60%) ya nafasi hizi iliwaendea wavulana ilhali wasichana wakapewa asilimia arubaini (40%) pekee. Matokeo ya shule zote mbili yanapojumlishwa, inadhihirika kuwa walimu waliwapatia wavulana nafasi kumi na tano (15) hii ikiwa ni asilimia sabini na moja nukta nne (71.4%) na wakawapa wsichana nafasi sita (6) pekee hi ikiwa ni asilimia ishirini na nane nukta sita (28.6%). Matokeo haya yanadhihirisha wazi wazi kuwa walimu waliwasaidia wavulana katika kuendeleza utawalaji dhidi ya wasichana kwa kuwapa nafasi nyingi pale ambapo wangeweza kuwapatia wanafunzi wote nafasi sawa.

Kigezo kingine kilichotumika katika kujua jukumu la mwalimu katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani, ni jinsi walimu walivyoteua wanafunzi pale ambapo idadi ya wavulana na wasichana walioinua mikono, haikuwa sawa. Kwa mfano, wakati ambapo ilitarajiwa kwamba mwalimu pengine angeteua msichana kwa sababu wasichana wengi zaidi kuliko wavulana walikuwa wameinua mikono, na hivyo kuwepo kwa uwezekano mkubwa wa wao kuteuliwa, mwalimu alifanya kinyume. Ilidhihirika kuwa mara nyingi wavulana waliteuliwa ingawaje uwezekano wao wa kuteuliwa ulikuwa mdogo kuliko uwezekano wa wasichana.

Katika shule "A" tunaona kuwa walimu waliwateua wavulana mara kumi na tisa (19) pale ambapo uwezekano wa wavulana kuteuliwa ulikuwa mdogo ukilinganishwa na uwezekano wa wasichana kuteuliwa, ilhali katika hali hiyo hiyo, wasichana wakateuliwa mara tisa (9) pekee. Hivyo wavulana walipata asilimia sitini na saba nukta tisa (67.9%) na wasichana, asilimia thelathini na mbili nukta moja (32.1%) pekee ya nafasi hizi.

Katika shule "B" mambo yalikuwa hayo hayo. Walimu waliwateua wavulana mara kumi na nane (18), hii ikiwa ni asilimia sitini na sita nukta saba (66.7%). Ilhali waliwateua wasichana mara tisa (9), hii ikiwa ni asilimia thelathini na tatu nukta tatu (33.3%). Matokeo

haya yanapojumlishwa, inakuwa kwamba walimu walionekana kuwapendelea wavulana. Kama inavyodhihirika katika jedwali 8 ukurasa wa 43, walimu katika hali hii, waliwateua wavulana mara thelathini na saba (37), na wasichana mara kumi na nane (18). Hivyo wavulana wakapewa asilimia sitini na saba nukta tatu (67.3%) ya nafasi hizi, ilhali wasichana wakapewa asilimia thelathini na mbili nukta saba (32.7%).

Tunaweza kukamilisha kwa kusema kuwa katika hali zote hizi wwalimu walionekana kuwapendelea wavulana, na hivyo basi, kuwasaidia katika kutawala mazungumzo ya darasani. Walimu, kama inavyodhihirika, wana jukumu katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ya darasani dhidi ya kikundi kimoja. Walimu, wanawapatia wavulana nafasi nyingi za kuzungumza hata pale ambapo uwezo wa wasichana na wavulana wa kupata nafasi ni sawa, au hata wakati ambapo uwezo wa wasichana ulikuwa mkubwa kuliko ule wa wavulana. Kwa hali zote zile, walimu waliwasaidia wavulana katika kutawala mazungumzo ya darasani.

Walimu, kwa hivyo, wana jukumu muhimu sana katika kuendeleza usawa wa mazungumzo ya darasani. Iwapo walimu wataelewa umuhimu wa mazungumzo na athari za utawalaji wa mazungumzo ya darasani dhidi ya kikundi kimoja, basi huenda wakajaribu kuhakikisha kuwa hakuna kikundi kitakacho faidi mazungumzo zaidi ya kingine. Kinyume na Whyte (ibid), anayesema kuwa ni vigumu kwa walimu kuwapatia nafasi sawa wasichana na wavulana katika mazungumzo ya darasani, utafiti huu umethibitisha kuwa, jambo hili linawezekana, hasa iwapo walimu wataelemishwa kuhusu umuhimu wa mazungumzo ya darasani. Kwa mfano katika shule "B", somo la Kiswahili kidato cha nne, mwalimu alifaulu katika kuwapa wasichana na wavulana nafasi sawa za kuzungumza. Unaposoma jinsi somo hili lilivyoendeshwa (Angalia kiambatisho xi uk 66), utagundua kuwa, mwalimu, kila alipompatia mvulana nafasi, nafasi iliyofuata, alimpa msichana.

3.3 Utaratibu wa kuteua wanafunzi katika mazunguzo ya darasani.

Utafiti huu ulibainisha kuwa, utaratibu uliotumika darasani wa kufundisha, kwa kiasi kikubwa uliendeleza utawalaji wa mazungumzo, ambapo wavulana walitawala mazungumzo hayo. Utaratibu uliotumika ni ule wa mwalimu kuanzisha mada, halafu ateua mwanafunzi kuzungumza, iwapo yeye mwalimu ameuliza swali. Baadaye, mwanafunzi alipojibu, mwalimu alizungumza tena au kuuliza swali jingine, halafu aliteua mwanafunzi mwingine. Utaratibu huu uliendelea hivyo mpaka pale kengele ilipolia, ambapo mwalimu alimaliza somo na kutoka darasani.

Utaratibu huu unasababisha walimu kutowapatia wanafunzi muda mwingi wa kuzungumza, aidha kwa kuuliza maswali au kujadiliana kati yao (yaani wanafunzi kwa wanafunzi). Utaratibu huu wa kufundishia, kama ilivyodhihirika katika utafiti huu, kwa kiasi kikubwa huendeleza utawalaji wa mazungumzo ambapo wavulana hutawala. Ilivyo ni kuwa utaratibu huu huwafaidi tu wavulana. Jambo hili huwaathiri vibaya wasichana kwani hawapati nafasi ya kuchangia na kujieleza kikamilifu katika mazungumzo ya darasani, hali twafahamu kuwa ni kupitia kwa mazungumzo ambapo, mbali na kuelewa mambo tofauti tofauti, huwa tunapitisha mawazo yetu, tunapokea mawazo ya wengine, na pia kuyathibitisha.

Kwa jumla, tunaweza kusema kuwa utaratibu uliotumika wa kuteua wanafunzi wanaposhiriki katika mazungumzo ya darasani, uliendeleza utawalaji ambapo wavulana walitawala mazungumzo hayo kwa kuchangia zaidi kuliko wasichana. Utaratibu huu uliwafaidi wavulana kwani wao ndio waliopata nafasi nyingi za kuzungumza. Katika utafiti huu, ilidhihirika kuwa kati ya madarasa manane ambayo mtafiti alichunguza, wavulana waliweza kufaidika na utaratibu huu, katika madarasa saba, ambapo walitawala mazungumzo

kwa kupata nafasi nyingi, ilhali ni katika darasa moja tu, ambapo wasichana na wavulana walichangia sawa kwa sawa katika mazungumzo.

3.4 Muhtasari

Katika sura hii, tumewasilisha matokeo ya utafiti huu, halafu tukafanya uchanganuzi. Tumewasilisha matokeo hayo katika majedwali tukizingatia misingi ya masomo na madhumuni ya utafiti. Kwanza, kwa kutumia swali la kwanza la utafiti, tumewasilisha matokeo katika jedwali linaloonyesha idadi ya nafasi na jumla ya maneno yaliyochangiwa na wanafunzi katika masomo ya Kiswahili na Kiingereza katika madarasa mbali mbali. Tumefanya hivyo kwa shule zote mbili. Baadaye tumewasilisha matokeo hayo katika jedwali linaloonyesha wastani wa maneno kwa kila nafasi, kwa shule zote mbili.

Pili, tumewasilisha matokeo ya utafiti huu katika majedwali mawili, kwa kuzingatia maswali mawili yaliyosalia ya utafiti. Katika majedwali haya, tumedhihirisha na kubainisha jinsi wasichana na wavulana wanavyoinua mikono katika kujibu maswali darasani, kina nani hawakuinua mikono, jinsi nafasi zilivyotumika, na jinsi walimu walivyoteua wanafunzi.

Mambo hayo yametuwezesha kujua ni nani walitawala mazungumzo ya darasani, majukumu ya wahusika katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ni yapi, na mwisho kubainisha iwapo utaratibu wa kuteua wanafunzi darasani uliendeleza utawalaji wa mazungumzo hayo.

SURA YA NNE

HITIMISHO

4.0 Utangulizi

Sura hii, inawasilisha, matokeo ya utafiti, mahitimisho ya utafiti, matatizo yaliyokumba utafiti huu na mwisho kutoa mapendekezo. Matokeo yamewasilishwa kutokana na maswali na madhumuni ya utafiti. Mahitimisho yamewasilishwa kutokana na matokeo ya utafiti na mwisho, matatizo na mapendekezo yametokana na matokeo ya utafiti.

Sura hii imegawanywa katika sehemu nne fupi fupi. Katika sehemu ya kwanza, tumewasilisha matokeo ya utafiti kwa muhtasari. Sehemu ya pili imewasilisha mahitimisho ya utafiti huu. Matatizo yaliyokumba utafiti huu yamejadiliwa katika sehemu ya tatu na mwisho mapendekezo yametolewa katika sehemu ya nne ya sura hii.

4.1 Matokeo ya utafiti.

Utafiti huu umebainisha kuwa wavulana ndio wanatawala mazungumzo ya darasani. Kwa kiasi kikubwa, imebainika kuwa wavulana ndio wanaopata nafasi nyingi za kuzungumza na kuchangia maneno mengi kuliko wasichana. Mbali na hivyo, wavulana wanakuwa na wastani mkubwa wa maneno kwa kila nafasi na pia wanafikisha na kupitisha wastani wa maneno kwa kila nafasi unaohitajika.

Utafiti huu pia umedhihirisha kuwa wasichana, wavulana na walimu wana majukumu katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo ambapo wavulana hutawala. Kwa mfano, wasichana hawainui mikono kwa wingi na hawatumii nafasi zao kikamilifu. Mambo haya husababisha wao kutochangia ipasavyo katika mazungumzo hali ambayo husababisha wao kutawaliwa katika mazungumzo ya darasani. Wavulana kwa upande wao huinua mikono mara nyingi na hivyo kupata nafasi nyingi za kuzungumza. Mbali na hivyo wanatumia nafasi

wanazopata kikamilifu na hivyo kuchangia zaidi katika mazungumzo. Mathalan, kutokana na uwezo wao wa kutumia ipasavyo nafasi wanazopata, wavulana wanatawala mazungumzo ya darasani.

Utafiti huu pia ulibainisha kuwa walimu 'waliwapendelea' wavulana kwa kuwapa nafasi nyingi na hivyo basi kuwasaidia katika kutawala mazungumzo ya darasani. Mwisho, utafiti huu umebainisha kuwa utaratibu unaotumika darasani wa kufundisha, kwa kiasi kikubwa unaendeleza utawalaji wa mazungumzo ambapo wavulana wanatawala mazungumzo hayo.

4.2 Hitimisho ya utafiti

Mazungumzo ni muhimu sana katika kujiendeleza kifikra na pia katika ujamiishaji. Wanaisimu wanakubaliana kwamba, mbali na kuwa mazungumzo ni muhimu katika upataji wa elimu, mazungumzo vilevile hutuwezesha kuendeleza mahusiano na pia hutusaidia katika kuendeleza uwezo wetu wa kuimudu lugha. Watafiti kama vile Mercer (1997) wamebainisha kuwa ni vigumu kuwaelimisha watu pasi kutumia lugha. Ni kutokana na mazungumzo ambapo watu wa lugha moja huweza kuwasiliana, kujifunza, kupitisha mawazo kwa wengine na kupokea mawazo mbali mbali.

Ingawaje katika mipango yake ya maendeleo ya mwaka wa 1996 serikali ilisisitiza kufutiliwa mbali kwa hali zinazodhihirisha ubaguzi wa umenke katika vitabu vya elimu na kusisitiza elimu bora kwa msichana, haikutaja swala la mazungumzo ya darasani ilhali imebainika kuwa mazungumzo ni muhimu katika upataji wa elimu. Tunachelea kwamba iwapo wasichana hawatashirikishwa kikamilifu katika mazungumzo ya darasani basi huenda wakaathirika katika upataji wa elimu. Hali hii pia huenda ikadhihirika katika jamii kwa jumla ambapo wanawake watakuwa watu wa kunyamaza tu katika jamii jambo ambalo huenda

likaathiri mahusianao yao na wanajamii kwa jumla. Si ajabu kwamba watoto watakaolelewa katika jamii kama hizi pia wakaathirika na kudhihirisha tabia hii darasani hivyo hali hii ikawa ni mzunguko.

4.3 Matatizo yaliyokumba utafiti

Kuna matatizo mawili makuu ambayo yalikumba utafiti huu. Tatizo la kwanza lilitokana na walimu. Baadhi ya walimu walikosa kuelewa lengo la utafiti na wakadhani kuwa walikuwa wakichunguzwa jinsi wanavyofunza. Jambo hili wakati mwingine lilisababisha walimu hawa kutoshirikiana kikamilifu na mtafiti. Kutokana na hali hii, ilimbidi mtafiti akae katika shule moja kwa muda mrefu zaidi ili kuweza kupata wasaa mwingi zaidi kuzoena na walimu hao, na hivyo kutoa uoga waliokuwa nao. Tatizo hili pia ilidhihirika miongoni mwa wanafunzi. Baadhi ya wanafunzi walikuwa na uoga na hiyo kutochangia ipasavyo. Jambo hili pia lilisababisha mtafiti kubaki nyanjani kwa muda mrefu kuliko alivyotarajia.

Tatizo la pili lililokumba utafiti huu, ni lile la vifaa vya utafiti. Wakati mwengine kinasa sauti kilikuwa mbali na wanafunzi na hivyo kukosa kunasa vyema baadhi ya mazungumzo ya wanafunzi. Isitoshe kuna wanafunzi wengine ambao walikuwa wakizungumza kwa sauti za chini kiasi kwamba hawakuwa wakisikika vyema. Hata hivyo, matumizi ya shajara za nyanjani yalisaidia sana katika hali kama hizi. Matatizo haya hata hivyo, hayakuathiri matokeo ya utafiti huu. Kama nilivyosema hapo mbeleni, suluhisho liliweza kupatikana kwa kukaa katika shule moja kwa muda wa kutosha, uliowezesha mtafiti kezoeana na walimu, na vile vile, matumizi ya shajara za nyanjani katika kusuluhisha tatizo la pili.

4.4 Mapendekezo

Matokeo ya utafiti huu, yamedhihirisha kuwa, kwanza, wavulana wanatawala mazungumzo ya darasani. Pili, wasichana hawashiriki kikamilifu katika mazungumzo ya darasani. Tatu, walimu huwasaidia wavulana katika kuendeleza utawalaji wa mazungumzo na mwisho, utaratibu unaoibuka wa kufundisha husaidia wavulana katika kutawala mazungumzo.

Kutokana na matokeo haya mtafiti ametoa mapendekezo yafuatayo. Kwa sababu walimu huwasaidia wavulana kutawala mazungumzo, yapaswa walimu hawa waelimishwe juu ya umuhimu wa kuwahusisha wasichana kikamilifu katika mazungumzo ya darasani. Ni kutokana na hali hii ambapo walimu wataweza kuwapatia wanafunzi wote darasani nafasi sawa za kuzungumza na hivyo wote kuchangia kikamilifu katika mazungumzo ya darasani.

Pili, mtafiti anapendekeza kuwa utafiti ufanywe kuchunguza ni kwa kivipi mwalimu anaweza kuwapatia wasichana na wavulana darasani, nafasi sawa za kuzungumza. Kwa mfano, katika utafiti huu, mwalimu mmoja katika darasa moja aliweza kuwapatia wasichana na wavulana nafasi sawa katika mazungumzo ya darasani. Je, walimu kama hawa hutumia mbinu gani? Je ni kwa sababu ya kuelewa mabo ya umenke ndiposa wanafanya hivyo? Mbali na hayo, utafiti kama huu ufanywe katika shule nyingi zaidi.

Mwisho, mtafiti anapendekeza kuwa, utafiti ufanywe kuhusu athari zinazotokana na utawalaji wa mazungumzo ya darasani. Ithibitishwe ni vipi kikundi kinachotawaliwa katika mazungumzo ya darasani, huathiriwa au kuhasirika.

VIAMBATISHO

Kiambatisho - i
Kiingereza Kidato cha tatu "A" (Jinsi wanavyopata nafasi na kuchangia)
Idadi ya wasichana: 18 (kumi na nane) **idadi ya wavulana**: 15 (kumi na tano)
Ws – Wasichana: **Wv** – Wavulana: + - kupata nafasi: - kutopata nafasi

Maswali ya mwalimu	Idadi ya walioinua mikono		Walioteuliwa kutokana na kuinua mikono		Walioteuliwa bila ya kuinua mikono		Wasiojibu baada ya kuteuliwa	
	Ws	**Wv**	**Ws**	**Wv**	**Ws**	**Wv**	**Ws**	**Wv**
Swali la 1	3	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 2	5	8	-	+	-	-	-	-
Swali la 3	5	4	+	-	-	-	-	-
Swali la 4	5	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 5	5	3	-	-	-	+	-	-
Swali la 6	1	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 7	0	6	-	+	-	-	-	-
Swali la 8	1	0	+	-	-	-	-	-
Swali la 9	1	0	+	-	-	-	-	-
Swali la 10	3	1	+	-	-	-	-	-
Swali la 11	3	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 12	0	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 13	0	1	-	+	-	-	-	-
Swali la 14	2	1	+	-	-	-	-	-
Swali la 15	2	1	+	-	-	-	-	-
Swali la 16	4	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 17	3	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 18	0	1	-	+	-	-	-	-
Swali la 19	2	1	+	-	-	-	-	-
Swali la 20	0	6	-	+	-	-	-	-
Swali la 21	1	5	+	-	-	-	-	-
Swali la 22	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 23	2	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 24	0	1	-	+	-	-	-	-
Swali la 25	2	1	-	+	-	-	-	-
Swali la 26	0	1	-	+	-	-	-	-
Swali la 27	0	1	-	+	-	-	-	-
Swali la 28	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 29	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 30	0	0	-	-	+	-	-	-
Swali la 31	0	0	-	-	+	-	+	-
Swali la 32	0	1	-	+		-	-	-
Swali la 33	0	0	-	-	+	-	-	-
Swali la 34	0	0	-	-	+		+	-
Swali la 35	0	0	-	-	-	+	-	-
Jumla	**50**	**60**	**11**	**14**	**4**	**6**	**2**	**0**

Kiambatisho - ii

Kiswahili kidato cha tatu "A" (jinsi wanavyopata nafasi na kuchangia)

Idadi ya wasichana: 18 (kumi na nane) **idadi ya wavulana**: 15 (kumi na tano)

Ws – Wasichana: **Wv** – Wavulana: + - kupata nafasi: - kutopata nafasi

Maswali	Idadi ya walioinua mikono		Walioteuliiwa kutokana na kuinua mikono		Walioteuliwa bila ya kuinua mikono		wasiojibu baada ya kuteuliwa	
	Ws	**Wv**	**Ws**	**Wv**	**Ws**	**Wv**	**Ws**	**Wv**
Swali la 1	0	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 2	1	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 3	2	1	+	-	-	-	-	-
Swali la 4	3	8	+	-	-	-	-	-
Swali la 5	5	4	+	-	-	-	-	-
Swali la 6	5	4	+	-	-	-	-	-
Swali la 7	6	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 8	0	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 9	3	0	+	-	-	-	-	-
Swali la 10	0	0	-	-	+	-	-	-
Swali la 11	4	3	-	-	+	-	-	-
Swali la 12	2	5	-	-	+	-	-	-
Swali la 13	6	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 14	0	0	-	-	+	-	+	-
Swali la 15	0	0	-	-	+	-	+	
Swali la 16	5	5	-	+	-	-	-	-
Swali la 17	3	7	-	+	-	-	-	-
Swali la 18	3	4	+	-	-	-	-	-
Swali la 19	5	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 20	5	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 21	4	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 22	3	1	-	+	-	-	-	-
Swali la 23	1	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 24	0	0	-	-	-	+	-	+
Swali la 25	0	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 26	0	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 27	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 28	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 29	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 30	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 31	0	1	-	-	+	-	-	-
Swali la 32	**Wote walijibu kwa pamoja bila kuinua mikono**							
Swali la 33	0	0	-	-	+	-	+	-
Swali la 34	0	1	-	+	-	-	-	-
Swali la 35	4	2	-	+	-	-	-	-

Swali la 36	0	0	-	-	+	-	+	-
Swali la 37	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 38	4	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 39	4	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 40	5	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 41	2	3	+	-	-	-	-	-
Swali la 42	2	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 43	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 44	2	1	-	-	-	+	-	-
Swali la 45	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 46	0	0	-	-	-	-	-	-
Swali la 47	2	5	-	+	-	-	-	-
Swali la 48	5	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 49	2	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 50	2	4	+	-	-	-	-	-
Swali la 51	4	3	+	-	-	-	-	-
Swali la 52	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 53	0	0	-	-	+	-	-	-
Jumla	**104**	**107**	**11**	**19**	**9**	**12**	**4**	**1**

Kiambatisho -iii

Kiswahili kidato cha nne "A" (Jinsi wanavyopata nafasi na kuchangia)

Idadi ya wasichana: 14 (kumi na nne) **idadi ya wavulana**: 16 (kumi na sita)

Ws – Wasichana: **Wv** – Wavulana: + - kupata nafasi: - kutopata nafasi

Maswali	Idadi ya walioinua mikono		Walioteuliwa kutokana na kuinua mikono		Walioteuliwa bila ya kuinua mikono		Wasiojibu baada ya kuteuliwa	
	Ws	**Wv**	**Ws**	**Wv**	**Ws**	**Wv**	**Ws**	**Wv**
Swali la 1	1	0	+	-	-	-	-	-
Swali la 2	6	5	-	+	-	-	-	-
Swali la 3	6	4	+	-	-	-	-	-
Swali la 4	4	6	+	-	-	-	-	-
Swali la 5	0	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 6	2	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 7	2	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 8	5	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 9	2	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 10	0	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 11	5	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 12	7	3	+	-	-	-	-	-
Swali la 13	0	5	-	+	-	-	-	-
Swali la 14	3	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 15	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 16	0	0	-	-	+	-	-	-
Swali la 17	4	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 18	2	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 19	4	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 20	0	1	-	+	-	-	-	-
Swali la 21	2	1	+	-	-	-	-	-
Swali la 22	3	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 23	3	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 24	0	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 25	4	3	+	-	-	-	-	-
Swali la 26	2	4	+	-	-	-	-	-
Swali la 27	**Wote walijibu kwa pamoja bila kuinua mikono**							
Swali la 28	0	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 29	5	5	-	+	-	-	-	-
Swali la 30	0	1	-	+	-	-	-	-
Swali la 31	1	1	-	+	-	-	-	-
Jumla	**73**	**78**	**10**	**18**	**1**	**1**	**0**	**0**

Kiambatisho - iv

Kingereza kidato cha nne "A" (Jinsi wanavyopata nafasi na kuchangia)

Idadi ya wasichana: 14 (kumi na nne) **idadi ya wavulana**: 16 (kumi na sita)

Ws – Wasichana: **Wv** – Wavulana: + - kupata nafasi: - kutopata nafasi

Maswali	Idadi ya walioinua mikono		Walioteuliwa kutokana na kuinua mikono		Walioteuliwa bila ya kuinua mikono		Wasiojibu baada ya kuteuliwa	
	Ws	**Wv**	**Ws**	**Wv**	**Ws**	**Wv**	**Ws**	**Wv**
Swali la 1	0	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 2	0	0	-	-	+	-	+	-
Swali la 3	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 4	-	-	**Wote walijibu kwa pamoja bila kuinua mikono**					
Swali la 5	2	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 6	0	0	-	-	+	-	-	-
Swali la 7	4	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 8	4	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 9	5	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 10	2	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 11	0	0	-	-	-	+	-	+
Swali la 12	0	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 13	2	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 14	4	3	+	-	-	-	-	-
Swali la 15	6	5	-	+	-	-	-	-
Swali la 16	-	-	-	-	-	+	-	-
Swali la 17	4	6	+	-	-	-	-	-
Swali la 18	5	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 19	2	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 20	2	3	+	-	-	-	-	-
Swali la 21	6	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 22	0	0	-	-	+	-	-	-
Swali la 23	0	2	-	-	-	+	-	-
Jumla	**21**	**29**	**5**	**10**	**3**	**4**	**1**	**1**

Kiambatisho - v

Kiingereza Kidato cha tatu "B"(Jinsi wanavyopata nafasi na kuchangia))

Idadi ya wasichana: 19 (kumi na tisa) **idadi ya wavulana**: 15 (kumi na tano)

Ws – Wasichana: **Wv** – Wavulana: + - kupata nafasi: - kutopata nafasi

Maswali	Idadi ya walioinua mikono		Walioteuliwa kutokana na kuinua mikono		Walioteuliwa bila ya kuinua mikono		Wasiojibu baada ya kuteuliwa	
	Ws	**Wv**	**Ws**	**Wv**	**Ws**	**Wv**	**Ws**	**Wv**
Swali la 1	0	0	-	-	+	-	-	-
Swali la 2	-	-	-	-	+	-	-	-
Swali la 3	-	-	-	-	+	-	-	-
Swali la 4	-	-	-	-	+	-	-	-
Swali la 5	-	-	-	-	+	-	-	-
Swali la 6	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 7	0	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 8	4	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 9	3	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 10	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 11	4	3	-	+	-		-	-
Swali la 12	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 13	3	4	+	-	-	-	-	-
Swali la 14	2	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 15	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 16	0	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 17	0	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 18	2	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 19	0	1	-	+	-	-	-	-
Swali la 20	3	2	+	-	-	-	-	-
Jumla	**21**	**29**	**3**	**8**	**5**	**4**	**0**	**0**

Kiambatisho - vi

Kiswahili kidato cha tatu "B"(Jinsi walivyopata nafasi na kuchangia))

Idadi ya wasichana: 19 (kumi na tisa) **idadi ya wavulana**: 15 (kumi na tano)

Ws – Wasichana: **Wv** – Wavulana: + - kupata nafasi: - kutopata nafasi

Maswali	Idadi ya walioinua mikono		Walioteuliwa kutokana na kuinua mikono		Walioteuliwa bila ya kuinua mikono		Wasiojibu baada ya kuteuliwa	
	Ws	**Wv**	**Ws**	**Wv**	**Ws**	**Wv**	**Ws**	**Wv**
Swali la 1	3	5	+	-	-	-	-	-
Swali la 2	4	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 3	4	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 4	2	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 5	3	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 6	2	0	+	-	-	-	-	-
Swali la 7	0	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 8	3	5	+	-	-	-	-	-
Swali la 9	2	1	-	+	-	-	-	-
Swali la 10	3	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 11	0	0	-	-	-	+	-	+
Swali la 12	1	0	+	-	-	-	-	-
Swali la 13	2	1	-	+	-	-	-	-
Swali la 14	0	0	-	-	+	-	-	-
Swali la 15	-	-	-	-	+	-	-	
Swali la 16	0	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 17	0	2	-	-	+	-	-	-
Swali la 18	-	-	-	-	+	-	-	-
Swali la 19	0	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 20	4	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 21	4	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 22	3	1	-	+	-	-	-	-
Swali la 23	4	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 24	3	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 25	0	0	-	-	+	-	+	-
Swali la 26	0	0	-	-	+	-	-	-
Swali la 27	1	1	+	-	-	-	-	-
Swali la 28	0	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 29	0	1	-	+	-	-	-	-
Swali la 30	3	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 31	2	3	+	-	-	-	-	-
Swali la 32	4	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 33	2	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 34	3	3	+	-	-	-	-	-
Swali la 35	3	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 36	0	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 37	2	3	+	-	-	-	-	-

Swali la 38	0	2	-	-	+	-	+	-
Swali la 39	0	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 40	1	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 41	0	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 42	1	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 43	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 44	4	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 45	0	1	-	-	-	+	-	-
Swali la 46	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 47	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 48	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 49	0	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 50	0	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 51	2	1	+	-	-	-	-	-
Swali la 52	2	1	-	+	-	-	-	-
Jumla	**77**	**89**	**14**	**27**	**7**	**7**	**2**	**1**

Kiambatisho – vii

Kiswahili kidato cha nne "B"(Jinsi walivyopata nafasi na kuchangia)

Idadi ya wasichana: 16 (kumi na sita) **idadi ya wavulana**: 19 (kumi na tisa)

Ws – Wasichana: **Wv** – Wavulana: + - kupata nafasi: - kutopata nafasi

Maswali	Idadi ya walioinua mikono		Walioteuliwa kutokana na kuinua mikono		Walioteuliwa bila ya kuinua mikono		Wasiojibu baada ya kuteuliwa	
	Ws	**Wv**	**Ws**	**Wv**	**Ws**	**Wv**	**Ws**	**Wv**
Swali la 1	3	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 2	4	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 3	0	3	-	-	-	+	-	-
Swali la 4	2	0	+	-	-	-	-	-
Swali la 5	3	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 6	0	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 7	3	0	+	-	-	-	-	-
Swali la 8	-	-	-	-	+	-	-	-
Swali la 9	**Mtafiti**							
Swali la 10	2	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 11	2	3	+	-	-	-	-	-
Swali la 12	3	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 13	**Wote walijibu kwa pamoja bila kuinua mikono**							
Swali la 14	**Wote walijibu kwa pamoja bila kuinua mikono**							
Swali la 15	**Wote walijibu kwa pamoja bila kuinua mikono**							
Swali la 16	2	3	+	-		-	-	-
Swali la 17	1	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 18	**Wote walijibu kwa pamoja bila kuinua mikono**							
Swali la 19	3	4	-	+	-	-	-	-
Jumla	**28**	**30**	**6**	**6**	**1**	**1**	**0**	**0**

Kiambatisho - viii

Kiingereza kidato cha nne "B"(Jinsi walivyopata nafasi na kuchangia)

Idadi ya wasichana: 16 (kumi na sita) **idadi ya wavulana**: 19 (kumi na tisa)

Ws – Wasichana: **Wv** – Wavulana: + - kupata nafasi: - kutopata nafasi

Maswali	Idadi ya walioinua mikono		Walioteuliwa kutokana na kuinua mikono		Walioteuliwa bila ya kuinua mikono		Wasiojibu baada ya kuteuliwa	
	Ws	**Wv**	**Ws**	**Wv**	**Ws**	**Wv**	**Ws**	**Wv**
Swali la 1	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 2	2	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 3	4	3	+	-	-	-	-	-
Swali la 4	0	0	-	-	+	-	+	-
Swali la 5	0	0	-	-	+	-	+	-
Swali la 6	0	0	-	-	-	+	-	-
Swali la 7	0	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 8	4	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 9	3	1	-	-	-	+	-	-
Swali la 10	2	3	+	-	-	-	-	-
Swali la 11	0	0	-	-	+	-	+	-
Swali la 12	0	0	-	-	-	+	-	+
Swali la 13	4	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 14	2	0	+	-	-	-	-	-
Swali la 15	2	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 16	5	4	-	+	-	-	-	-
Swali la 17	2	4	+	-	-	-	-	-
Swali la 18	0	1	-	+	-	-	-	-
Swali la 19	3	5	-	+	-	-	-	-
Swali la 20	2	2	+	-	-	-	-	
Swali la 21	3	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 22	2	3	-	+	-	-	-	-
Swali la 23	0	2	-	+	-	-	-	-
Swali la 24	4	2	+	-	-	-	-	-
Swali la 25	3	3	+	-	-	-	-	-
Swali la 26	4	3	-	+	-	-	-	-
Jumla	**51**	**50**	**8**	**11**	**3**	**4**	**3**	**1**

Kiambatisho ix
Jinsi walivyochangia shule "A" na "B" kwa jumla

Ws – Wasichana: **Wv** – Wavulana:
Ks3 – Kiswahili kidato cha tatu: **Kn3** – Kiingereza kidato cha tatu: **Ks4** – Kiswahili kidato cha nne
Kn4 – Kiingereza kidato cha nne: **Ws** – wasichana: **Wv** - Wavulana

		SHULE "A"					SHULE "B"					
		Ks 3	**Kn 3**	**Ks 4**	**Kn 4**	**Jumla A**	**Ks 3**	**Kn 3**	**Ks 4**	**Kn 4**	**Jumla B**	**Jumla A + B**
Nafasi kutokana na kuinua mikono	**Ws**	11	11	10	5	**37**	14	3	6	8	**31**	**68**
	Wv	19	14	18	10	**61**	24	8	6	11	**49**	**110**
Nafasi kutokana na kutoinua mikono	**Ws**	9	4	1	3	**17**	7	5	1	3	**16**	**33**
	Wv	12	6	1	4	**23**	7	4	1	4	**16**	**39**
Jumla ya nafasi zote	**Ws**	20	15	11	8	**54**	21	8	7	11	**47**	**101**
	Wv	31	20	19	14	**84**	31	12	7	15	**65**	**149**
Nafasi ambazo hazikutumika	**Ws**	4	2	0	1	**7**	2	0	0	3	**5**	**12**
	Wv	1	0	0	1	**2**	1	0	0	1	**2**	**4**
Nafasi walizopewa ingawaje wachache waliinua mikono	**Ws**	4	1	2	2	**9**	4	1	2	2	**9**	**18**
	Wv	8	4	4	3	**19**	10	2	1	5	**18**	**37**
Mara ambazo waliinua mikono	**Ws**	30	18	21	12	**81**	29	7	11	17	**64**	**145**
	Wv	33	24	27	16	**100**	38	11	11	19	**79**	**179**
Mara ambazo hawakuinuaa mikono	**Ws**	22	17	9	9	**57**	20	9	2	9	**40**	**97**
	Wv	19	11	3	5	**38**	11	5	2	7	**25**	**63**
Nafasi walizopewa kulipokuwa na idadi sawa ya walioinua mikono	**Ws**	0	1	1	0	**2**	2	0	0	2	**4**	**6**
	Wv	2	0	5	2	**9**	2	0	2	2	**6**	**15**
Idadi ya maneno yaliyochangiwa	**Ws**	29	67	29	28	**153**	36	41	100	51	**228**	**381**
	Wv	74	174	65	87	**400**	69	64	97	105	**336**	**736**
Jumla ya mikono iliyoinuliwa	**Ws**	104	50	73	42	**269**	77	21	30	51	**179**	**448**
	Wv	107	60	78	50	**295**	89	29	28	50	**196**	**491**

Kiambatisho x
Idadi ya wasichana na wavulana katika utafiti

	Shule "A"		**Shule "B"**	
	Wavulana	Wasichana	Wavulana	Wasichana
Kidato cha 3	15	18	15	19
Kidato cha 4	16	14	19	16
Jumla 3+4	**31**	**32**	**34**	**35**

Kiambatisho – xi:
Shule "B" Kiswahili kidato cha nne

Tarehe:2/2/01 **Somo**: Kiswahili **Kidato**: 4 (Nne) **Mwalimu**: Bw. Kombe **Uana**: Mume
Idadi ya wasichana: 16 (kumi na sita) **idadi ya wavulana**: 19 (kumi na tisa)
Muda – Dakika 35 (Thelathini na tano)
MAELEZO:
Msisitizo katika mabano – maelezo au idadi ya wanaoinua mikono

Msisitizo na mlazo – majibu ya wanafunzi yatakayotumika katika uchanganuzi.
Ms – Msichana: **Ws** – wasichana: **Mv** – mvulana: **Wv** – Wavulana
Ach. --Achaguliwa

Unasaji ulianza mwanzo wa somo

1. **Mwalimu**: Leo tuna mgeni ambaye ametutembelea na atakuwa na sisi darasani na kuangalia jinsi tunavyosoma. Nataka musome makala hayo niliyowapatia halafu tujibu maswali yanayofuata. Nawapa dakika kumi na tano haya anzeni. (**Baada ya kusoma anauliza maswali**) Makala hayo yanahusu nini? (**Ws - 3: Wv -3: Ach. Mv**)
   Mv: ***Makala haya yanahusu sayansi ya kutumbisha***

2. **Mwalimu**: Vyema, Sayansi ya Kutumbisha. Kwa hivyo, sayansi ya kutumbisha na madhara yake ndio inayoelezwa hapa. Nataka mpitie hayo maswali mpaka mwisho, halafu tuyajibu. (**Wanasoma maswali tena**) Inua mkono unipe jibu la swali la kwanza. Andika kichwa kifaacho cha makala hii (**Ws - 4:Wv -2 : Ach. Ms**)
   Ms: ***Kichwa kifaacho cha makala hii ni sayansi ya kutumbisha.***

3. **Mwalimu**: Sayansi ya kutumbisha, vyema, wakati unapoandika jibu la swali hili andika aidha kwa kutumia herufi kubwa katika maneno yote au kila neno muhimu lianze na herufi kubwa. (**Aandika ubaoni**)...Swala la kutumia sayansi ya kutumbisha linaweza kumsaidia binadamu mabaa gani mawili yanayotukabili sasa? Swali hili nampa mvulana si lazima * wale ambao wameinua mikono hata wale ambao hawakuinua. (**Ws –0:Wv –3)** Wewe hapo (**Ach. Mv**)
   Mv: ***Itaondoa janga la kiangazi***

4. **Mwalimu**: Mwingine atwambie baa la pili? (**Ws - 2: Wv -0**) Msichana sasa (**Ach. Ms**)*
   Ms: ***Itaondoa uhaba wa mashamba***

5. **Mwalimu**: Kwa hivyo itaondoa uhaba wa mashamba. Hmm ...kwa hivyo haya majanga mawili yataisha. Maswali sasa ni yale ambayo unasoma swali na unafikiria kwa makini. Kila mmoja asome swali la tatu tena. Kila mmoja nitampatia nafasi atoe maoni yake*. Swali linasema unadhani ni kwa nini wanyama waliozalishwa kutumia sayansi hii bado wako mahabarani? Kila

mmoja nitampatia nafasi, mvulana, msichana, mvulana msichana. Aliye tayari ni nani? **(Ws -3 :Wv -2)** Haya anza **(Ach. Mv)**

Mv: ***Wanyama wengi waliozalishwa kwa kutumia sayansi hii ni wadogo wadogo hivyo basi huhifadhiwa katika mahabara ili kuendeleza mbele utafiti.***

6. **Mwalimu**: Hatuwezi kuwatumia kwa chakula **(Ws - 0: Wv -2: Ach. Mv)**
   Mv: ***Hatuwezi mwalimu.***

7. **Mwalimu**: Hatuwezi kwa sababu wanyama ni wadogo wadogo. Hilo ni wazo zuri sana. Lazima tujue kwamba mtahini anakutaka mawazo yako kulingana na vile unaelewa ujumbe wa mwandishi. Tupate msichana* sasa tupate mawazo yake. **(Ws - 3:Wv - 0:**) Gladys? **(Ach. Ms)** Unadhani ni kwa nini wanyama waliozalishwa kwa kutumia sayansi hii ya kutumbisha bado wangali mahabarani?
   Ms: ***Mimi naona kama ambaye yani bado wako kule kwenye mahabara kwa sababu wale wanasayansi bado wanafanya utafiti zaidi kulingana na vile wale wanyama kama kwa kweli wanaweza kuwa wakubwa***

8. **Mwalimu:** Endelea
   Ms: ***Yaani maoni yangu ni kwamba wale wanyama bado wamewekwa kwenye mahabara kwa sababu wanasayansi bado wanafanya utafiti zaidi kulingana na vile wale wanyama ikiwa kweli wanaweza kunenepa na kuwa wakubwa.***

9. **Mwalimu:** Yaani anatwambia hivi, wale wanyama ... hili ni wazo zuri sana **(Kengele yalia mwalimu amgeukia mtafiti)** siju Bwana kengele imelia tuendelee ama pengine...?

Mtafiti: Tuendelee

10. Mwalimu: Katika swali hili, hapa mtahini anakutaka mawazo yako hivyo yote yanaweza kufaa iwapo utajieleza vilivyo. Hapa kunafuata swali la matumizi ya lugha. habari hii. Ikiwa unaweza kutoa ufafanuzi inua mkono **(Ws - 2: Wv - 2: Ach. Mv)** Naam?
   Mv: ***Methali hii kutamba kwingi ni kuondoka na mavi inamaanisha kuwa ukizidisha kufanya kitu kupita kiasi kitu hicho chaweza kukuletea madhara***

11. **Mwalimu:** Tunapata wazo kuwa ukizidisha kitu hata kama kina uzuri fulani **(Kelele nyingi kutoka nje hivyo hasikiki vizuri)** ...kwa hivyo hapa mwandishi hapa anatutahadharisha kuhusu uvumbuzi wa aina hii. Hilo ni wazo zuri ambalo lakubalika mwengine atupatie ufafanuzi wake **(Ws - 2: Wv -3: Ach .Ms)** Naam?
   Ms: ***Maarifa mengi yanaweza kuleta madhara***

12. Mwa**limu:** Maarifa? Kweli? **(Ws – 3:Wv - 2: Ach. Ms)**
   Ms: ***Ndio, ukiwa na maarifa mengi yanaweza kuleta madhara***
13. Mwalimu: Ndio vizuri sana, kuna ule msemo unaosema sijui akili nyingi huondoa... **(Wajibu kwa jumla)**

Jumla:Maarifa

14. **Mwalimu**: Hivyo mwandishi anasisitiza kuwa akili nyingi huondoa maarifa. Si tukienda zaidi tunashindana na Mungu? *(***Wajibu kwa jumla***)*

Jumla:Ndio

15. **Mwalimu**: ... basi kuoana kutakuwa na haja gani ikiwa kama una haja na watoto unaenda katika "lab" unatengeza watoto je hii famili unity kwa Kiingereza itakuwepo tena?

Jumla:Hapana

16. **Mwalimu**: Hivyo kutumia sayansi hii kuna madhara zaidi... kutokana na wakati, nataka tumalize hilo swali la 'a', kuna ubaya gani kutumbisha watu? Mtahini hapa anakutaka mawazo yako. Kupitia sayansi hii kuna ubaya gani kutumbisha watu? Kutumbisha wanyama ni sawa je itakuwaje ikiwa tutatumbisha binadamu? (**Ws – 2:Wv - 3: Ach. Ms**) Naam Gladys?

Ms: ***Tunaona ubaya wa kutumbisha kutakuwa hakuna haja ya kuoana kwa hivyo mtu... (Hasikiki) kutakuwa hakuna kuoana.***

17. **Mwalimu:** Huo sio ubaya twataka utoe ule ubaya. Kuna ubaya gani kutumbisha watu? Hapa ni kila mmoja atoe maoni yake uwanja uko wazi. (**Ws - 1: Wv - 4: Ach. Mv**)

Mv: ***Nafikiri ubaya wa kutumbisha watu ni kuwa yule binadamu anaweza kuwa (Hasikiki) ama atakuwa na akili na maarifa mengi kupita wengine.***

18. **Mwalimu**: Ni kuwa unaweza kutumbisha mhalifu na hivyo huo ni ubaya ama kwa mfano Hivyo ubaya upo na uzuri upo. Tumeelewana? (**Wajibu wote**)

Jumla:Ndio

19. **Mwalimu:** ...atakuwa ni mtu kutokana na mahabara hatakuwa na ubinadamu. Swali la mwisho. Mwandishi anaonekana kutishwa sana na uwezekano wa sayansi ya kutumbisha kuishia mikononi mwa wendawazimu weledi kwani kuna hatari gani? (**Ws - 3:Wv - 4: Ach. Mv**)

Mv: ***Kutumbisha kuishia mikononi mwa weledi wendawazimu weledi kuna madhara kwa mfano, Hitler angejua sayansi hii basi angetumbisha wanajeshi wengi tena wale wa kinyama ili kupigana vita.***

20. **Mwalimu**: Vizuri sana Swali hilo linataka uangalifu zaidi katika kutoa sababu na hatari unazoziona. Nafikiri tutachia hapo kwa leo kwani wakati umekwisha.

(Mwisho wa somo)

Kiambatisho – xii
Shule "A" Kiingereza kidatao cha tatu

Tarehe: 31/01/01 **Somo**: Kiingereza **Kidato**: 3 (Tatu) **Mwalimu**: Masha **Uana**: Mume
Idadi ya wasichana: 15 (kumi na tano) **idadi ya wavulana**: 18 (kumi na nane)
Muda – Dakika 35 (Thelathini na tano)
MAELEZO:
Mlazo katika mabano – tafsiri:
Msisitizo katika mabano – maelezo au idadi ya wanaonyosha mikono
Msisitizo na mlazo – majibu ya wanafunzi yatakayotumika katika uchanganuzi.
Ms – Msichana: **Ws** – wasichana: **Mv** – mvulana: **Wv** - Wavulana
Ach.-Achaguliwa
(Unasaji ulianza mwanzo wa somo)

1. **Mwalimu**: Today we shall try to discuss the characters in the play 'The Burdens'. Who are
   the characters in this book? (*Leo tutazungumzia juu ya wahusika katika mchezo wa 'The Burdens'. Wahusika ni kina nani katika kitabu hiki)*
   (Ws – 3: Wv – 2: Ms Acha.)
   Ms: ***Tinka***

2. **Mwalimu**: Next? *(Mwingine?)* **(Ws – 5: Wv – 8 Mv Acha.)**
   Mv: ***Wamala***

3. **Mwalimu**: Another one? *(Muhusika mwingine?)* **(Ws –5: Wv – 4: Ms Acha.)**
   Ms: ***Kaija***

4. **Mwalimu**: Another character? *(Muhusika mwengine?)*
   (Ws – 5: Wv – 4: Mv achaguliwa)
   Mv: ***Nyakake***

5. **Mwalimu**: Yes, another character? *(Sawa muhusika mwengine?)*
   (Ws – 5: Wv – 3:achaguliwa Mv ambaye hakunyosha mkono)
   Mv: ***Vincent***

6. **Mwalimu**: Next? *(Mwingine?)* **(Ws – 1: Wv – 0: Ach. Mv ambaye hakunyosha mkono)**
   Mv: ***Yankees***

7. **Mwalimu**: Another character? *(Muhusika mwingine?)* **(Ws – 0: Wv – 6: Mv achaguliwa)**
   Mv: ***Yankees secretary***

8. **Mwalimu**: Well, another one? *(Sawa, mwingine?)* **(Ws – 1: Wv – 0: Ms achaguliwa)**
   Ms: ***The nun***

9. **Mwalimu**: ...what does she say about Wamala *(...anasema nini kuhusu Wamala)* **(Ws-1: Wv-0: achaguliwa Ms)**
   Ms: ***she tries to tell Tinka that their father has gone for a burial*** *(Anajaribu kumwambia Tinka kwamba baba yao ameenda mazishini)*
10. **Mwalimu**: What does Wamala say? *(Wamala anasema nini?)* **(Ws-3: Wv-1: Acha. Ms)**
   Ms: ***Wamala says that Tinka has gone to see other women*** *(Wamala anasema kuwa Tinka ameenda kuona wanawake wengine)*

11. **Mwalimu**: What are the traits of Wamala *(Wamala alikuwa mtu wa aina gani?)* **(Ws-3: Wv-2: Ms achaguliwa)**
   Ms: ***He was adamant*** *(Alikuwa hakubali kushinndwa)*

12. **Mwalimu**: Why do we say that ...was drunkard? *(Kwa nini tunasema ...alikuwa mlevi)* **(Ws-0: Wv-2: Mv achaguliwa)**
   Mv: ***He fought with his wife because of enguli*** *(alipigana na mkewe kwa sababu ya enguli)*

13. **Mwalimu**: Another reason? *(Sababu nyingine?)* **(Ws-0: Wv-1: achaguliwa Mv)**
   Mv: ***He was drunk because we are told that one day he came home when he was drunk and demanded beer from Tinka and Tinka refused to give the beer but he got it from where it was hidden.*** **(***Alikuwa mlevi kwa sababu tunaambiwa kwamba siku moja alikuja nyumbani akiwa mlevi na akataka apewe pombe na Tinka na Tinka akakataa kumpa pombe lakini akaichukua kutoka pale ilipokuwa imefichwa***)**

14. **Mwalimu**: ...what are the basic needs? *(Mahitaji ya kimsingi ni yapi?)* **(Ws-2: Wv-1: achaguliwa Ms)**
   Ms: ***Food*** *(Chakula)*

15. **Mwalimu**: Yes another need? *(Ndio, hitaji jingine la kimsingi?)* **(Ws-2:Wv-1:Acha. Ms)**
   Ms: ***Shelter*** *(Makao)*

16. **Mwalimu**: Another basic need, yes? *(Hitaji jingine la kimsingi)* **(Ws-4:Wv-3: Acha. Mv)**
   Mv: ***Clothes*** *(Mavazi)*

17. **Mwalimu**: Are you sure? Well another need? *(Una hakika? Hitaji jingine?)* **(Ws-3: Wv-2: Acha. Mv)**
   Mv: ***Education*** *(Elimu)*

18. **Mwalimu**: I don't think that is a basic need. Well what are Wamala's other traits? *(Sidhani kama hilo ni la kimsingi. Naam Wamala alikuwa na hali gani nyingine?)* **(Ws- 0: Wv- 1: Acha. Mv)**

Mv: ***Unfaithfulness because he was sleeping with other women*** *(Hakuwa mwaminifu kwa sababu alikuwa akitembea na wanawake wengine)*

19. **Mwalimu**: Yes another trait? *(Naam hali nyingine?)* **(Ws- 2: Wv-1: Acha. Ms)**
    Ms: ***Wamala was poor because he was not able to buy a new bed*** *(Alikwa maskini kwa sababu hakuweza kununua kitanda kipya)*

20. **Mwalimu**: Are you sure that is a reason for saying that Wamala was poor? … well another trait *(una hakika hiyo ni sababu ya sisi kusema kwamba Wamala alikuwa maskini? Naam nini tena?)* **(Ws- 0: Wv- 6: Acha. Mv)**
    Mv: ***He was corrupt, this is because we are told he didn't bother about his family*** *(Alikuwa mfisadi kwa sababu tunaambiwa kwamba hakuishughulikia jamii yake)*

21. **Mwalimu**: I don't think that is true… so, another trait? *(Sidhani kuwa hiyo ni kweli, hali nyingine?)* **(Ws-1: Wv – 5: Acha. Ms)**
    Ms: ***He was proud*** *(Alikuwa na kiburi)*

22. **Mwalimu**: Can you explain? **(Hajibu)** Well another trait? *(Unaweza kufafanua? Hali nyingine?)* **(Ws-0: Wv-0: Acha. Mv)**
    Mv: ***He was a fearful person because*** **(Anyamaza haendelei)** *Alikuwa mtu wa kuogofya…*

23. **Mwalimu**: Another one? *(Nyingine?)* **(Ws – 2: Wv – 2: Acha. Ms)**
    Ms: ***He was a businessman*** *(Alikuwa mfanyi biashara)* ***(Wanafunzi wengine wacheka)***

24. **Mwalimu**: I don't think that is true another trait? *(Sidhani kama hiyo ni kweli hali ngingine?)* **(Ws – 0:Wv – 1: Acha. Mv)**
    Mv: ***He was violent because we find that in the passage, Wamala strikes Tinka with a bottle of liquor.(Alikuwa mpenda vita kwa sababu tunaona katika makala, Wamala anampiga Tinka na chupa ya pombe)***

25. **Mwalimu**: Well that is fine, can we get other instances where we find Wamala's violence? *(Naam, tunaweza kupata hali nyingine zinzoonyesha kuwa Wamala alipendela vita?)***(Ws –2: Wv – 1: Acha. Mv)**
    Mv: ***He wanted to fight the clerk who cheated him that he would employ his daughter.*** *(alitaka kumpiga yule karani aliyemdanganya kwamba angemuajiri kazi msichana wake)*

26. **Mwalimu**: Any other instance? *(Hali nyingine?)* **(Ws – 0: Wv – 1: Acha. Mv)**
    Mv: ***When they play, Tinka threatens Wamala that the police are coming then Wamala holds Tinka by the neck.***(*Wakati wanapocheza, Tinka anamshtua Wamala kwamba polisi wanakuja, hii inasababisha Wamala kumkaba koo Tinka*)

27. **Mwalimu**: Any other trait? **(Ws – 0: Wv – 1: Acha. Mv)**
    Mv: ***Wamala was revengeful he had to seduce a catholic nun away from the convent.*** *(Wamala alikuwa mtu wa kulipiza kisasi kwani alimtorosha mtawa wa kikatoliki kutoka katika jumba la watawa)*

28. **Mwalimu**: Yes any other trait?*(Naam hali nyingine?)* **(Ws – 0: Wv – 0: Acha. Mv)**
    Mv: ***Wamala was sympathetic because when he hurts Tinka's elbow, he washed and then applied medicine on it.*** *(Wamala alikuwa mtu wa huruma kwani hata baada ya kujeruhi kisukusuku cha Tinka alimuosha halafu akampaka dawa)*

29. **Mwalimu**: Hmm, another trait? *(Hmm, hali nyingine)* **(Ws – 0: Wv – 0: Acha. Mv)**
    Mv: ***Wamala was poor because when his daughter was sick he did not take her to hospital.*** *(Wamala alikuwa maskini kwa sababu mtoto wake wa kike alipokuwa mgonjwa hakumpeleka hospitali)*

30. **Mwalimu**: I don't think that is a trait, yes *(Sidhani kama hiyo ni hali. Naam?)* **(Ws – 0: Wv – 0: Acha. Ms)**
    Ms: ***Ambitious, Wamala was not satisfied of being a minister he wanted to become a president.*** *(Alikuwa mpenda makuu hakutosheka na kuwa waziri bali alitaka kuwa rais)*

31. **Mwalimu**: Now can you tell me why was Wamala jailed? You there *(Sasa nataka muniambie kwa nini Wamala alifungwa gerezani? Wewe hapo)* **(Ws – 0: Wv – 0: Acha. Ms)**
    Ms: **(anyamaza kimya hajibu)**

32. **Mwalimu**: Yes? *(Naam?)* **(Ws –0: Wv – 1: Acha. Mv)**
    Mv: ***He was jailed because of love*** *(Alifungwa gerezani kwa sababu ya mapenzi)*

33. **Mwalimu**: Love of what? Can somebody be jailed because of love? I don't think that is
    true. Now tell me, is Wamala corrupt? *(Mapenzi ya nini? Mtu anaweza kufungwa kwa sababu ya mapenzi? Sidhani kama hiyo ni kweli sasa niambieni, Wamala alikuwa mfisadi?)* **(Hakuna anayenyosha mkono)** Mercy?
    Ms: ***No***

34. **Mwalimu**: Why do you say no? Mercy? *(Kwa nini unasema la? Mercy?)*
    Ms: **(Anyamaza kimya hajibu)**

35. **Mwalimu**: Yes Juma? *(Naam Juma?)*
    Mv: ***He is corrupt because after he was given the chance of being a president instead of making up his mind and proceed with his political ...*****(Anyamaza haendelei yaelekea alichanganyikiwa)** *(Alikuwa mfisadi kwa sababu hata baada ya kupewa nafasi ya kuwa rais badala ya kukubali aliendelea na siasa...)*

36. **Mwalimu**: Well it seems you cant answer that, think about it and when we meet again tomorrow you should be able to answer that. *(Inaonekana mmeshindwa na kujibu swali hilo. Nataka mulifikirie na kesho tukikutanatena, muwe munaweza kulijibu)*

(Mwisho wa somo)

Kiambatisho – xiii
Shule "A" Kiswahili kidato cha tatu

Tarehe:31/1/01 **Somo**: Kiswahili **Kidato**: 3 (Tatu) **Mwalimu**: Mr. Mwangome **Uana**: Mume
Idadi ya wasichana: 15 (kumi na tano) **idadi ya wavulana**: 18 (kumi na nane)
Muda – Dakika 35 (Thelathini na tano)
MAELEZO:
Msisitizo katika mabano – maelezo au idadi ya wanaonyosha mikono
Msisitizo na mlazo – majibu ya wanafunzi yatakayotumika katika uchanganuzi.
Ms – Msichana: **Ws** – wasichana: **Mv** – mvulana: **Wv** – Wavulana
Ach.- Achaguliwa
Unasaji ulianza mwanzo wa somo

1. **Mwalimu:** Leo tutazungumzia juu ya sentensi na vipengele vyake. Je kama mnakumbuka, sentensi ni nini? **(Ws – 0: Wv – 4)** Naam? **(Ach. Mv)**
   Mv: ***Sentensi ni kipande cha maneno)***

2. **Mwalimu:** Tulisema kwamba katika sentensi hatuna kipande cha maneno, badala yake tuna nini? **(Ws – 1: Wv – 4: Ach. Mv)**
   Mv: ***Fungu la maneno lenye maana maalum.***

3. **Mwalimu:**Kuna aina ngapi za sentensi? **(Ws – 2: Wv – 1: Ach. Ms)**
   Ms: ***Tatu***

4. **Mwalimu:**Nani ataziainisha? **(Ws – 3:Wv – 8: Ach. Ms)**
   Ms: ***Fupi***

5. **Mwalimu:**Fupi, hmm **(Ws – 5:Wv – 4)** Matilda? **(Ach. Ms)**
   Ms: ***Neno moja***

6. **Mwalimu:**Aina nyengine? **(Ws – 5 Wv – 4: Ach. Ms)**
   Ms: ***Sentensi ndefu***

7. **Mwalimu:**...nani atatupa mfano wa sentensi fupi? **(Ws – 6: Wv–3: Ach. Mv)**
   Mv: ***Ninaandika.na kalamu nyeusi.***

8. **Mwalimu:**Hiyo sentensi ina makosa gani? **(Ws – 0: Wv –4: Ach. Mv)**
   Mv: ***Matumizi ya 'na' na 'kwa' ingekuwa, ninaandika kwa kalamu nyeusi.***

9. **Mwalimu:** Vizuri sana. Je sentensi ya neno moja, **(Ws – 3: Wv – 0)** Naam? **(Ach. Ms)**
   Ms: ***Ninaandika.***

10. **Mwalimu:** Vizuri sana. Sentensi ya mseto, **(Ws – 0: Wv – 0)** Priscilla? **(Acha. Ms)**
   Ms: ***Ninaandika kwa kalamu nyeusi katika daftari langu***

11. **Mwalimu:** Vizuri, sasa nataka muniambie kuna ipi na ipi za maneno? **(Ws–4:Wv– 3)** Irene? **(Ach. Ms ambaye hakunyosha mkono)**
   Ms: ***Kiima***

12. **Mwalimu:** Aina nyingine? **(Ws – 2: Wv – 5)** Naam wewe? **(Ach. Ms ambaye hakunyosha mkono)**
   Ms: ***Kitenzi***

13. **Mwalimu:** Mfano wa sentensi yenye kitenzi? **(Ws – 6: Wv – 4: Ach. Mv)**
   Mv: ***Baba amekula chakula***

14. **Mwalimu:** Amekula? Hiyo amekula inaonyesha kiima na kitenzi? Ina viambishi lakini haina maneno ambayo yanasimamia mambo haya. Tunataka fungu la maneno ambalo litakuwa na kiima na kitenzi. **(Hakuna anayenyosha mkono)** Labda turudie ule mfano wetu. Deche? **(Ach. Ms)**
   Ms: **(Akaa kimya bila kujibu)**

15. Mwalimu: Nataka turejelee mfano wetu. **(Hakuna anayenyosha mkono)** Irene? **(Ach. Ms)**
   Ms: **(Akaa kimya bila kujibu)**

16. **Mwalimu:** Naam? **(Ws – 5: Wv – 5: Ach. Mv)**
   Mv: ***Ninaandika kwa kalamu***

17. **Mwalimu:** Moja kwa moja tunaona kuwa sentensi hiyo inacho kiima. Kiima kikiwa nini nini? **(Ws –3: Mv Wv – 7: Ach. Mv)**
   Mv: ***kalamu***

18. **Mwalimu:** Kitenzi? **(Ws –3: Wv – 4: Ach. Ms)**
   Ms: ***Ninaandika***

19. **Mwalimu:** Hivyo tunaona kwamba sentensi hii imejumuisha kiima na kitenzi. Katika sentensi ya neno moja, labda vipengele hivyo vitawakilishwa na vile tunavyoviita viambishi. Katika neno "ninaandika", nani atatwambia kiambishi cha kwanza? Naam? **(Ws-5: Wv-3: Ach. Mv)**
   Mv: ***Ni***

20. **Mwalimu:** Ikiwa kina maana gani? **(Ws – 5: Wv – 2: Acha. Mv)**
   Mv: ***Nafsi***

21. **Mwalimu:** Nafsi gani? **(Ws – 4: Wv – 4: Ach. Mv)**
*Mv: **Nafsi ya kwanza***

22. **Mwalimu:** ...ingawaje...kiambishi kingine? **(Ws – 3: Wv – 1: Ach. Mv)**
*Mv: **Na***

23. **Mwalimu:** Ikiwa na maana gani? **(Ws – 1: Wv – 0: Ach. Mv ambaye hakunyosha mkono)**
*Mv: **Wakati***

24. **Mwalimu:** Wakati gani? Wakati uliopo? Tulisema kwamba katika sentensi, wakati inasimamiwa na kipengele gani cha maneno? ? **(Ws – 0: Wv – 0)** Nzaro **(achaguliwa Mv)**
Mv: **(Hajibu kitu abaki kimya)**

25. **Mwalimu:** Tulisema sentensi ina maneno mawili, kiima na kitenzi. Yale mengine yote yanasaidia Kiima au kitenzi, hivyo, wakati unasaidia nini? **(Ws –0: Wv – 3: Ach. Mv)**
*Mv: **unasaidia kiima***

26. **Mwalimu:** Kwa hivyo kulingana na wewe, wakati ni nini? Ni jina, ni kivumisha au ni kielezi? **(Mv yule yule ajibu)**
*Mv: **Kielezi***

27. **Mwalimu:** Kama ni kielezi kinasaidia nini? Ikiwa neno linasaidia kitenzi linakuwa nini? **(Ws – 0: Wv – 0: Mv bila kunyosha mkono ajibu)**
*Mv: **kielezi***

28. **Mwalimu:** Kielezi, kwa hivyo, wakati hapa inakuwa nini? Ni kielezi au ni kivumishi? **(Ws – 0: Wv – 0: Ach. Mv)**
*Mv: **Ni kielezi***

29. **Mwalimu:** Kiambishi kingine? **(hakuna anayenyosha mkono)** Imani? **(Ach. Mv)**
*Mv: **Naandika***

30. **Mwalimu:** Naandika, kweli? **(Ws – 0: Wv – 0)** Kule nyuma Tom? **(Ach. Mv)**
*Mv: **Andik***

31. **Mwalimu:** Sasa tunaona kwamba tuna kiambishi andik, kwa nini si andika? **(Ws–0:Wv –1)** Emma? **(Ach. Ms)**
*Ms: **Kwa sababu...** **(Hasikiki)***

32. **Mwalimu:** Naam utaona kwamba... kwa mfano, neno hili linaweza kuwa andika, andikwa, andikisha...jinsi ya kufanya katika hali gani? **(wote wajibu ka jumla)**

Jumla: kufanya

33. **Mwalimu**: Kundi la kwanza litakuwa fungu tenzi na kundi la pili fungu nomino. Ni vipi tunaweza kujua fungu nomino? **(Ws – 0: Wv – 0)** Mbalazi? **(Ach. Ms lakini hajibu)**
    Ms: **(Anyamaza kimya)**

34. **Mwalimu**: Naam? **(Ws – 0: Wv – 1)** Kaingu? **(Ach. Mv)**
    Mv: ***Fungu tenzi huwa limejaa vitenzi***

35. **Mwalimu**: Kwa hivyo tunaweza kuwa na vitenzi vingapi katika fungu tenzi? **(Ws – 4: Wv – 2: Ach. Mv)**
    Mv: ***Viwili***

36. **Mwalimu**: Kufikia hapa tunataka tupambanue sentensi hii. **(aashiria sentensi ubaoni)** Sentensi hii iko katika fungu gani? **(Ws – 0: Wv – 0)** Karisa Jane? **(Ach. Ms)**
    Ms: **(Anyamaza kimya)**

37. **Mwalimu**: Naam? **(Ws – 0: Wv – 0)** Franklin? **(Ach. Mv)**
    Mv: ***iko katika fungu tenzi***

38. **Mwalimu**: Iko katika fungu tenzi kwa sababu gani? Inaeleza kuhusu kuandika. Huku kuandika ndiko muhimu kwa sababu anaeleza ninaandika... Tupambanue maneno katika sentensi hii neno andika linawakilisha nini? **(Ws – 4: Wv – 2: Ach. Ms)**
    Ms: ***Kitenzi***

39. **Mwalimu**: Kitenzi, naam, kalamu? **(Ws – 4: Wv – 2: Ach. Ms)**
    Ms: ***Jina***

40. **Mwalimu**: Nyeusi? **(Ws – 5: Wv – 2: Ach. Mv)**
    Mv: ***Kielezi***

41. **Mwalimu**: Tulisema kazi ya kielezi katika sentensi ni nini? **(Ws – 2: Wv – 3: Ach. Ms)**
    Ms: ***chaeleza kuhusu kitenzi***

